# Nipashe

**Ijumaa Agosti 26, 2022** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581049

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




China na Tanzania katika ushirikiano wa kiuchumi kwa maendeleo endelevu — Ukurasa 14

Tupongezane kwa sensa ya amani na utulivu ila... — Ukurasa 13

VIFURUSHI VYA UTT-AMIS — Ukurasa 12

Silaha 'vyuma vinapobana,'mkwamo mdororo kiuchumi

BUFE

IJUMAA AGOSTI 26, 2022 Nipashe BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

BIASHARA

ASA yawatangazia wakulima habari njema ya kumaliza uhaba wa mbegu

Na Renatha Msungu

UKURASA 11


SUPA JACKPOT

TZS. 1,025,118,259

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Mbowe:** Mrema alikuwa mwenye uthubutu, kufanya uamuzi mgumu

UKURASA 3



# Wataka uwazi matumizi tozo

• **Taasisi** yabainisha umuhimu wake kwa maendeleo... *Endelea ukurasa 2*



Mkurugenzi wa Idara ya Diaspora wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi James Bwana (kulia) na Ofisa Mkuu wa Wateja Wakubwa na Serikali wa Benki ya NMB, Alfred Shao, wakibadilishana hati jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini makubaliano ya ufadhili wa matengenezo ya mfumo wa kidigitali wa kutunza taarifa za diaspora. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MWALIMU AFARIKI DUNIA AKIAMULIA UGOMVI WA JIRANI**

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Taisi Kata ya Bumera, mkoani Mara, Ibrahimu Maryoba...

**Miili watu watatu iliyokutwa katika viroba yazikwa kaburi moja**

UKURASA 3

# Mdee na wenzake kuhojiwa kortini leo

UK.2


**MICHEZO** | **YANGA YATAJA MECHI 3 NGUMU** UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Mdee na wenzake kuhojiwa kortini leo

**Na Waandishi Wetu**

MBUNGE wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake saba wanatarajia kuhojiwa leo kuhusu viapo vyao katika shauri walilofungua kupinga kuvuliwa uanachama na Baraza Kuu la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Uamuzi wa kuitwa na kuhojiwa ulitolewa Mahakama Kuu Masijala Kuu mbele ya Jaji Cyprian Mkeha baada ya Wakili wa CHADEMA, Peter Kibatala, kuwasilisha maombi hayo na mahakama ikakubali.

Wakili Kibatala aliomba mahakama iwape wabunge hao hati za wito ili wafika mahakamani leo ambayo ni siku ya usikilizwaji wa shauri hilo na wawahoji.

Mbali ya Mdee, wabunge wengine wanaotakiwa kufika mahakamani ni Nusrat Hanje, Grace Tendega, Esther Matiko, Jesca Kishoa, Cecilia Pareso, Esther Bulaya na Hawa Mwaifunga

Mawakili wa wabunge hao, Aliko Mwamanenge na Ipilinga Panya walidai wakishafaili viapo kinzani, wataona kama ipo haja ya kuwaita mahakamani baadhi ya viongozi wa CHADEMA kuwahoji.

Awali Jaji Mkeha aliwataka wajibu maombi kuwasilisha mahakamani viapo kinzani Agosti 5, mwaka huu, huku mawakili wa kina Mdee wakitakiwa kuwasilisha hoja za nyongeza Agosti 10, 2022.

Mdee na wenzake 18 walifungua shauri hilo Julai 21, mwaka huu, mahakamani huko dhidi ya CHADEMA, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wakipinga uamuzi wa Baraza Kuu la chama hicho kuwavua uanachama Mei 11, 2022.

Katika shauri hilo namba 36 la mwaka 2022, wabunge hao pamoja na mambo mengine, wanaiomba mahakama hiyo ipitie mchakato na uamuzi huo wa kuwafukuza kisha itoe amri tatu.

Wabunge hao wanaomba mahakama itengue mchakato na uamuzi wa kuwavua uanachama, iwalazimishe CHADEMA kuwapa haki ya kuwasikiliza na amri ya zuio dhidi ya Spika wa Bunge na NEC kukuchukua hatua yoyote mpaka malalamiko yao yatakapotolewa uamuzi.

Uamuzi huo wa Baraza Kuu ulitokana na rufani walizozikata Mdee na wenzake kupinga uamuzi wa awali wa kuwavua uanachama uliotolewa na Kamati Kuu, Novemba 27, 2020, iliyowatia hatiani kwa kosa la kwenda kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum bila ridhaa ya chama.

Mdee anadai kuwa sababu iliyotolewa na Baraza Kuu kumfukuza uanachama ilitokana na makosa yasiyo na maana na yasiyoweza kuthibitika, kuwa alikula njama kujiteua mwenyewe na kuapa kuwa mbunge wa viti maalum.

Kina Mdee pamoja na mambo mengine, wanadai kuwa mchakato na uamuzi wa kuwafukuza uanachama haukuzingatia matakwa ya kisheria na misingi ya haki, wakidai kuwa hawakupewa haki ya kusikilizwa.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipata maelezo ya moja ya kitabu kinachoelezea historia na kumbukumbu ya Oman na Zanzibar kutoka kwa Mwenyekiti wa Mamlaka ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa ya Oman, Dk. Hamed Mohd Al Dhawiani (katikati) na Balozi Mdogo wa nchi hiyo, anayefanyia kazi zake kisiwani humo, Said Salim Al Sinawi, wakati wa mazungumzo yao, Ikulu, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Wananchi wataka uwazi wa matumizi tozo miamala simu

**Maulid Mmbaga na Loyce Cyriacus (SJMC)**

TAASISI isiyo ya kiserikali ya TWAWEZA imesema utafiti uliofanyika hivi karibuni unaonyesha kwamba wananchi wengi wanataka uwazi katika matumizi ya fedha za miamala ya simu.

Akiwasilisha taarifa ya utafiti huo jana Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TWAWEZA, Aidan Eyakuze, alisema wananchi wengi waliohojiwa, wameiomba serikali kuweka bayana matumizi ya fedha zinazotokana na tozo ili hata wanapokatwa wajue kwamba zinakwenda wapi.

Eyakuze alisema Watanzania wengi wako tayari kulipa tozo iwapo wangepata taarifa kuhusu matumizi ya fedha hizo huku baadhi wakionyesha kuwa wanajua pesa zinatumikaje na kwamba wanaweza kutafuta kwa urahisi taarifa kutoka serikalini juu ya matumizi ya mapato ya tozo.

"Maoni ya wananchi kuhusu tozo za miamala ya fedha kwa njia ya simu yanatofautiana. Wengi wanakubali kuwa tozo hiyo ni njia muhimu ya serikali kukusanya mapato na kwamba inasaidia kumfanya kila mtu achangie maendeleo ya taifa," alisema Eyakuze.

Aliongeza kuwa wachache walikubali kwamba tozo hizo zitapunguza utegemezi kwa wafadhili pia ni kitu kizuri lakini huku wengine wamebainisha kuwa wangeunga mkono zaidi tozo hizo iwapo wangekuwa na taarifa kamili kuhusu matumizi yake.

Kwa mujibu wa Eyakuze, wananchi wanataja miradi mbalimbali ambayo wangependa itekelezwe kutokana na tozo za miamala, ikiwamo huduma za afya, elimu, ujenzi wa barabara, maji, umeme, kilimo na mikopo.

**MWENENDO WA NCHI**

Utafiti pia, kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, unaonyesha kwamba katika miezi sita iliyopita, sekta ya elimu imeboreshwa kwa asilimia 68, uhuru wa kujieleza asilimia 60, hali ya kisiasa (56), ulinzi na usalama (59), kupungua unyanyasaji dhidi ya wanawake (61) na watoto asilimia 60.

Alibainisha kuwa asilimia 68 ya wananchi walisema gharama za maisha zimepanda zaidi katika kipindi hicho, huku wakisema upatikanaji wa ajira na fursa za kujipatia riziki zimepungua kwa asilimia 48.

"Kwa ujumla wananchi wengi wanasema nchi iko kwenye mwelekeo mzuri kwa asilimia 30, 25 wanasema haiko kwenye mwelekeo sahihi huku 44 wakionyesha kuwa hawajui kuhusu mwelekeo wa nchi," alisema.

"Matumaini ya wananchi kuhusu suala la uchumi yako chini, idadi ya wanaosema hali ya uchumi ni mbaya ni mara nne ya wale wanaosema uchumi ni mzuri," alisema Eyakuze.

**GHARAMA ZA BIDHAA**

Alisema utafiti unaonyesha kuwa duniani kote bei za bidhaa zinaongezeka ikiwamo Tanzania ambapo alibainisha kuwa ndani ya miaka miwili kutoka Machi 2021 hadi Machi 2022 gharama ya mahindi imeongezeka kwa asilimia 21, mchele (34), maharage (tatu), petroli (31) na Dizeli asilimia 30.

Alisema kwa mujibu wa utafiti, bei ya mahindi katika mikoa mbalimbali nchini imeongezeka ndani ya miaka miwili ikiwamo Arusha asilimia 42, Dar es Salaam (54), Dodoma (790, Mtwara (30) na Mwanza 15.

"Wananchi wanasema hali ya ugumu wa maisha ni moja ya matatizo yanayowakabili kwa sasa na unasababishwa na kupanda kwa gharama za maisha, kukosekana kwa ajira na fursa za kuingiza kipato, njaa na uhaba wa chakula, vituo duni vya afya, upatikanaji wa maji safi, huduma duni ya usafiri na ubora wa elimu," alisema Eyakuze.

Aliongeza kuwa utafiti ulibainisha kwamba ukosefu wa chakula kwa mkoa wa Dar es Salaam unasababisha ugumu wa maisha kwa asilimia tisa, mikoa mingine (21) na vijijini (30). Alisema inashangaza kuonyesha kwamba kiwango kikubwa cha vyakula huzalishwa vijijini lakini ndiko kunakoongezeka kwa uhaba wa huduma hiyo.

Pia alisema walipowauliza wananchi juu ya nini wanapenda serikali zao za mitaa ziwafanyie, walijibu kwamba wanahitaji kushughulikiwa kwa huduma duni za usafiri, vituo vya afya, maji na gharama za maisha. Hatua hiyo, alisema inatoa picha kuwa jamii ina uelewa mkubwa kuhusu majukumu ya serikali za mitaa.

Alieleza kuwa wananchi pia walitoa wito kwa Rais kushughulikia kupanda kwa gharama za maisha, kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, usafiri na fursa za kujipatia kipato.



Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Scheiner (kulia), akihesabiwa na karani wa sensa ya watu na makazi, nyumbani kwake, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# Mbowe: Mrema alikuwa na uthubutu, uamuzi mgumu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MWILI wa aliyekuwa Mwenyekiti wa Tanzania Labour Party (TLP), Augustino Mrema (77), umezikwa nyumbani kwake Ngugha, Kijiji cha Kiraracha wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro huku Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, akimtaka ni kielelezo bora cha watu wenye uthubutu.

Katika salamu zake za rambirambi wakati wa maziko hayo jana, Mbowe alisema Mrema alikuwa kiongozi mwenye uwezo wa kufanya uamuzi mgumu.

"Alikuwa ni mtu wa misimamo, ameacha jina kubwa katika nchi, ameigusa kila kona. Sisi wenzake wana mageuzi tumepita nchi nzima na tumeona nyayo zake. Sisi tunajifunza mambo mengi kutoka kwake.

"Mungu akawape subira TLP wakati wanakwenda kujaribu kuziba pengo la Mrema, watangulize upendo, wamtegemee Mungu, safari hiyo siyo rahisi," Mbowe alisema.

Katika maziko hayo, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Kanali mstaafu Ngemela Lubinga, alisema kifo cha Mrema kimeacha pengo katika medani za siasa kwa sababu alikuwa mzalendo wa kweli.

"Mrema japo ameondoka lakini alipokuwa hai, alitimiza hitaji lake kulingana na mahitaji ya dunia na dunia inavyokwenda," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachawene, akitoa salamu za serikali katika msiba huo, alisema:

"Kwa niaba ya serikali inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, ninaleta kwenu salamu zake, Makamu wa Rais, Mzee (Dk. Philip) Mpango, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwingi na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wamenituma niwaletee salamu zao.

"Kipekee sana sisi kama serikali tuna kila sababu ya kukiri matendo mema aliyoyafanya, hatuwezi kusahau mchango wake katika ujenzi wa siasa na demokrasia. Ana rekodi kubwa katika siasa za upinzani, lazima tuyaenzi yale aliyoyafanya wakati wa uhai wake. Ameacha mengi kama alama."

Waziri Simbachawene alisema Mrema amefariki dunia akiwa Mwenyekiti wa Bodi ya Parole, hivyo serikali itamuenzi kwa kuwa amefanya kazi kubwa na ndiyo Rais Samia akamtuma kwenda katika maziko hayo kwa kuwa shughuli zote za siasa ziko chini ya wizara yake.

"Mrema aliwahangaikia watu maskini, wanawake waliokuwa wakipigwa na waume zao wanakumbuka mzee (Mrema) aliwatetea na wanaume mnajua balaa lake. Ni mtu aliyewatetea zaidi wanyonge, hakuwa mtu aliyetetereka katika imani yake," alisema.

Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei, alisema kifo cha Mrema ni msiba wa taifa kwa kuwa kuna mambo matatu muhimu ya wanasiasa wa Tanzania na hasa vijana kujifunza kwake.

"Tunapopewa wajibu wa kuutumikia umma, tutumike kwa upendo na uaminifu. Hakuna ambaye hajaguswa na kifo cha Mrema kwa sababu alihubiri wakati wote haki, amani na mshikamano. Alipenda na aliamini sana suala la usawa wa kijinsia, wanawake wanajua, hakika amecha alama.

"Mrema alijua kwamba madaraka yanatoka kwa bwana na hakuwa mtu wa kujivuna na wala hakuwahi kuitukana serikali wakati alipokuwa anafanya siasa," alisema.

Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Mohamed Ally Ahmed, alisema Mrema alikuwa muumini wa demokrasia ya kweli na alikuwa anakwenda na maono yake.

"Hakuwa mtu wa kugombana, kusukumana na aliamini demokrasia, alitumikia vyama vya siasa vitatu, alipoona watu wanagombana na kung'ang'ania vyeo, aliondoka na kuhamia kwingine kutafuta kile anachokiamini ili kuungwa mkono," alisema.

**MAZIKO YALIVYOKUWA**

Nipashe ilishuhudia maelfu ya waombolezaji katika safari hiyo ya mwisho duniani kwa Mrema, huku vilio vikitawala baada ya mwili wake kuwekwa nje ya nyumba yake kwenye eneo maalum la ibada saa 6:20 mchana kuruhusu mwakilishi wa Askofu wa Jimbo Katoliki la Moshi, Padri Deogratius Matiika, kuongoza ibada ya maziko.

Halikuwa jambo rahisi kwa familia yake na waombolezaji kuzuia hisia zao, kukishuhudiwa na Nipashe makundi ya waombolezaji yaliyojumuisha wananchi wa mikoa mbalimbali, viongozi wa serikali, viongozi wa dini na wanasiasa nyumbani kwa Mrema.

Makundi hayo yalikuwa yakijadili maisha ya kisiasa ya mwanasiasa huyo nguli na mchango wake katika medani za siasa na hasa ngome ya upinzani nchini.

# Miili watu iliyokutwa katika viroba yazikwa kaburi moja

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WATU watatu wanaodaiwa kuwa wafanyabiashara ya madini, ambao waliuawa na kutupwa wakiwa kwenye viroba katika Wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, wamezikwa kwenye kaburi moja.

Maziko ya miili hiyo yalifanyika katika maeneo ilikookotwa ikiwa imetupwa na watu wasiojulikana katika kitongoji cha Dibabara, Kijiji cha Msamvu, Kata ya Tunguli, wilayani humo, ilizikwa juzi katika kaburi moja.

Jana, Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Abel Busalama, alisema serikali imefikia uamuzi huo baada ya miili hiyo kutotambuliwa kwa zaidi ya wiki mbili sasa.

"Ni kweli marehemu hao wamezikwa jana (juzi) katika makaburi yaliyoko eneo la Kitongoji cha Kwasebe Kata ya Songe wilayani hapo baada ya kukaa hospitalini kwa wiki mbili bila kutambuliwa wala kupatikana kwa ndugu.

"Ni kweli miili ya watu hao imezikwa lakini halmashauri ndiyo wenye maelezo zaidi kuhusiana na kuwahifadhi marehemu hao," alisema Busalama.

Pamoja na miili hiyo kuzikwa, alisema bado vyombo vya usalama vinaendelea na jitihada za kuwabaini na kuwakamata waliyohusika na tukio la mauaji hayo ya kinyama huku akisisitiza kuwa uchunguzi wa awali unaonyesha unyama huo umefanywa na watu nje ya wilaya ya Kilindi.

"Tunawataka wananchi wanapohisi gari au watu, mashaka hayo yasipuuzwe na badala yake wajiridhishe na inapotokea hofu basi wawasiliane haraka na viongozi wa eneo husika ili kudhibiti vitendo kama hivi vya kihalifu," alisema Busalama.

Msimamizi wa chumba cha kuhifadhia maiti katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Kilindi ya Songe, Athuman

Kisalazo, alisema miili ya watu hao ilizikwa juzi majira ya saa 1:00 usiku kwenye makaburi ya Kwasebe jirani na hospitali hiyo.

Kisalazo alisema watu hao walizikwa katika kaburi moja kwa alama maalumu za herufi ya A na B kama ilivyoelekezwa na uongozi.

Awali akizungumzia tukio hilo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Tunguli, Omary Mtoi, alisema Agosti 11 majira ya saa 1:00 usiku, wakazi wa kitongoji Dibabara ambao ni jamii ya wafugaji, waliona gari rangi nyeupe aina ya Toyota Land Cluser likiingia maeneo ya kitongoji hicho na kushusha viroba viwili ambavyo hawakugundua vilikuwa na nini ndani.

Mtoi alisema asubuhi siku iliyofuata, wananchi hao waligundua kuwa viroba vilivyotupwa vilikuwa na miili ya watu.

Alisema baada ya kugundua, walitoa taarifa kwenye uongozi wa kitongoji, kata na polisi ambao walifika na kwa kuwa marehemu hao hawakufahamika maeneo hayo waliipeleka miili hiyo katika machimbo ya Seita ambako pia hawawatambui.




# Mwalimu afariki dunia akiamulia ugomvi wa jirani

**Na Samson Chacha,** TARIME

MWALIMU Mkuu wa Shule ya Msingi Taisi Kata ya Bumera, mkoani Mara, Ibrahimu Maryoba, amefariki dunia kutokana na shinikizo la damu wakati akienda kuamua ugomvi wa jirani yake.

Akizungumza na Nipashe kuhusu tukio hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Sokoni, Moi Buruma, alisema majira ya usiku akiwa nyumbani kwake Kitongoji cha Nyairoma, Ibrahimu alikwenda kuamulia ugomvi kwa jirani yake aliyetajwa kwa jina moja la Juma aliyekuwa na ugomvi na mke wake.

Mwenyekiti huyo alisema jirani yake alipiga kelele za kuomba msaada, ndipo mwalimu huyo alipotoka na kwenda kuamua ugomvi huo na alipofika nje alianguka na kupoteza fahamu.

Alisema wasamaria wema walijitokeza na kumbeba kumpeleka Kituo cha Afya Sirari kwa ajili ya kupata matibabu, lakini alifariki wakati akihudumiwa.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Kanda Maalum Tarime Rorya, ACP Geofrey Sarakikya, alisema: "Ni kweli kumetokea kifo cha mwalimu huyo na taarifa za mganga zinaonyesha alifariki kutokana shinikizo la damu, mishipa ya damu ilipasuka na kuvuja kwa ndani na kusababisha kifo chake."

"Tunaendelea na uchunguzi zaidi na tunawaomba wananchi kuacha kueneza mambo yasiyo na uhakika badala yake wafuate mambo ya kitaalamu kama anavyoeleza mganga wa kituo cha afya kwamba mwalimu huyo alifariki kutokana na shinikizo la damu."

Mwili wa mwalimu huyo ulipelekwa Hospitali ya Wilaya ya Tarime kufanyiwa uchunguzi, ulirejeshwa nyumbani kwake katika Kitongoji cha Nyairoma, Kijiji cha Sokoni na unatarajiwa kuzikwa leo.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitia saini kitabu cha maombolezo wakati alipohani msiba wa Celia Mwambe, ambaye ni mtoto wa Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe, nyumbani kwake, Kinondoni jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

## Mtoto aliyefariki kwenye bwawa la kuogelea kuzikwa leo

**Na Romana Mallya**

MWILI wa Cellie Mwambe (14), mtoto wa Mbunge wa Jimbo la Ndanda, Cecil Mwambe, aliyefariki dunia baada ya kujirusha kwenye bwawa la kuogelea nyumbani kwao, Ada Estate, Kinondoni, Dar es Salaam, umesafirishwa kwenda Ndanda wilayani Masasi kwa maziko.

Misa ya mazishi ilifanyika jana katika Kanisa la St. Peter, Oysterbay na kuongozwa na Paroko wa Kanisa hilo, Alister Makubi na baadaye kusafirishwa kuelekea Mtwara kwa ajili ya maziko yanayotarajia kufanyika leo.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alifika nyumbani kwa mbunge huyo kuhani msiba huo.

Cellie alifariki dunia Jumanne baada ya kujirusha kwenye bwawa la kuogelea nyumbani kwao akiwa anacheza na wenzake na kujigonga chini.

Mwanafunzi wa kidato cha pili, St. Mary Mazinde Juu, Celine Nicole aliiambia Nipashe kuwa, Cellie alikuwa mchapakazi na alipenda kusaidia wengine na alikuwa kiongozi wa darasa.

Juzi, Mbunge Cecil akizungumza na East Africa Radio, alisema mtoto wake alikuwa akicheza na bahati mbaya wakati wakikimbizana na wenzake aliruka ndani ya maji akaenda upande wenye kina kidogo akagonga chini akashindwa kujisaidia na kunywa maji mengi.

"Kulikuwa hakuna watu wazima karibu wa kumwokoa, akanywa maji walipokuja kumwokoa alifikishwa hospitali ikashindikana.

"Sikuwapo nilikuwa safari, alikunywa maji mengi na alifia hospitalini, alipata huduma kama saa mbili akafariki dunia, walimfikisha hospitali saa tisa alasiri na alifariki saa 11 jioni," Mbunge Cecil alisema.

Mwalimu wa darasa wa mwanafunzi huyo, Charles Bajuta alikuwa Cellie alikuwa mtoto mzuri, kiongozi, alipenda kushirikiana na wengine na kuwaunganisha na hakupenda uzembe.

"Alikuwa mwanafunzi mwenye ubora kitaaluma, uongozi yupo vizuri mno, mchangamfu, ni mwanafunzi ambaye unakaa naye na usichoke, anakwambia mwalimu hiki au kile, kwa kweli sijaamini, ila Mungu amempenda zaidi," alisema.

## Wanachama 13 wa ACT wajitosa ubunge EALA

**Romana Mallya na Lissa Chanya (UDOM)**

WANACHAMA 13 wa Chama cha ACT-Wazalendo wamejitokeza kugombea ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) kwenye mchakato huo uliofungwa juzi.

Katibu wa Idara ya Kampeni na Uchaguzi ACT-Wazalendo, Mohammed Massaga, alisema jana kuwa majina ya wagombea watakaokidhi sifa na vigezo yatawasilishwa kwenye kikao cha Kamati Kuu ya chama kinachotarajiwa kukutana kwa siku mbili kuanzia Septemba 2 mwaka huu.

"Hadi muda wa kuchukua na kurejesha fomu unakamilika, wanachama waliojitokeza kuchukua na kurejesha ni 13 (wanawake wanne)," ilisema taarifa hiyo.

Alisema waliogombea ni pamoja na Ado Shaibu, Emmanuel Mvula, Twaha Taslima, Mbaraka Chilumba, Esther Thomas, Halima Nabalang'anya, Jafet Massawe, Hamza Mtunu, Said Rashid, Fungo Benson, Godbless Msofe, Dk. Nasra Omar na Pavu Juma.

Alisema kuwa baada ya hatua hiyo ya kuchukua na kurejesha fomu, majina ya wagombea yatawasilishwa kwenye sekretarieti ya chama taifa kuchunjwa kwa kuzingatia sifa na vigezo vya kisheria na kikanuni vinavyoongoza mchakato huo.

Massaga alisema baada ya mchujo huo ndipo majina yenye sifa yatawasilishwa kwenye kikao cha Kamati Kuu ya chama kinachotarajiwa kukutana siku mbili kuanzia Septemba 2, mwaka huu jijini Dar es Salaam kwa ajili ya uteuzi wa mwisho.

"Kwa mujibu wa Katiba ya ACT-Wazalendo Ibara ya 79(1) (xvii), Kamati Kuu ya chama ndicho chombo chenye madaraka ya kuthibitisha uteuzi wa wagombea wa ubunge wa Afrika Mashariki kwa tiketi ya chama," alisema.

Aliongeza kuwa majina ya wagombea watakaoteuliwa na Kamati Kuu, yatawasilishwa bungeni kwa hatua ya mwisho ya uchaguzi.

**"Hadi muda wa kuchukua na kurejesha fomu unakamilika, wanachama waliojitokeza kuchukua na kurejesha ni 13 (wanawake wanne)," ilisema taarifa hiyo.**

TANGAZO

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

**CHUNYA DISTRICT COUNCIL**

# AUDITED FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2021

| | Notes | 2021 TZS ' | 2020 TZS ' |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 22 | 1,010,740,473 | 916,858,953 |
| Receivables and prepayments | 23 | 978,064,781 | 776,730,160 |
| Inventories | 24 | 605,117,745 | 651,603,686 |
| Other financial assets | 25 | 14,550,875 | 7,152,125 |
| | | **2,608,473,875** | **2,352,344,924** |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 25 | 76,553,000 | 76,553,000 |
| Property, plant and equipment | 26 | 24,080,864,159 | 25,200,311,311 |
| Work in Prgress | 26 | 3,822,158,704 | |
| Investment Properties | 27 | 523,920,000 | 408,000,000 |
| | | **28,503,495,863** | **25,684,864,311** |
| **TOTAL ASSETS** | | **31,111,969,736** | **28,037,209,234** |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 28 | 334,079,386 | 674,161,076 |
| Current Portion of Long-term borrowings | 30 | 64,475,577 | 64,475,577 |
| Employee benefits | 31 | 1,684,595,290 | 2,277,156,537 |
| Deferred income (Grant) | 11 | 83,561,336 | 44,679,481 |
| | | **2,166,711,589** | **3,060,472,671** |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Long-term borrowings | 30 | 69,382,394 | 64,475,577 |
| Deferred Capital (Grant) | 33 | 326,394,281 | 354,774,377 |
| | | **395,776,675** | **419,249,954** |
| **TOTAL LIABILITIES** | | **2,562,488,264** | **3,479,722,625** |
| **NET ASSETS** | | **28,549,481,474** | **24,557,486,609** |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated surplus | | 28,472,928,474 | 24,480,933,608 |
| MCR | | 76,553,000 | 76,553,000 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | **28,549,481,474** | **24,557,486,608** |

Hon. Bosco S. Mwanginde
Council Chairperson
Date: 28.9.2021

Tamimu Kambona
Council Director
Date: 28.9.2021

MWENYEKITI WA HALMASHAURI CHUNYA

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR CHUNYA DISTRICT COUNCIL

## CASH FLOW STATEMENT FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Note | 2021 TZS ' | 2020 TZS ' |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| ***Receipts*** | | | |
| Taxes and levies | 45 | 2,573,036,100 | 2,107,850,128 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 46 | 1,217,932,401 | 1,423,627,276 |
| Revenue grants received | 48 | 18,049,176,360 | 16,039,343,091 |
| Revenue from exchange transactions | 47 | 129,950,700 | 74,796,398 |
| Women, youth and disability loans Recovery | 54 | 322,115,900 | 127,422,500 |
| Other revenue | 49 | - | 138,794,550 |
| Change in Deposit account | 22 | (72,669,212) | 71,170,162 |
| ***Payments*** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 50 | (13,625,247,541) | (12,597,514,192) |
| Supplies and consumables used | 51 | (3,665,086,762) | (4,566,396,455) |
| Maintenance expenses | 53 | (697,825,684) | (634,161,371) |
| Grants and other transfer payments | 20 | (519,445,980) | (381,013,861) |
| Women, youth and disability Loans issued | 54 | (604,500,000) | (71,000,000) |
| Cash taken by Treasury at the year-end | 11&33 | | (39,157,106) |
| Election fund return to Treasury | 11 | | (9,564,462) |
| TASAF fund return to Treasury | | (6,490,000) | |
| **Net cash from operating activities** | | **3,100,946,283** | **1,684,196,659** |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Acquisition of property, plant, and equipment & investment properties | 55 | (3,007,766,688) | (1,406,047,130) |
| Advances and loans made to other parties | | - | - |
| **Net cash from investing activities** | | **(3,007,766,688)** | **(1,406,047,130)** |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Cash proceeds from other short or long-term borrowings; | 30 | 34,865,763 | 139,463,051.00 |
| Loan Repayment | 30 | (30,064,177) | (21,523,218) |
| Interest Charged | 30 | (4,099,661) | (2,934,984) |
| **Net cash used in financing activities** | | **701,925** | **115,004,849** |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | **93,881,520** | **393,154,378** |
| **Net foreign exchange difference** | | - | - |
| **Cash and cash equivalents at beginning of period** | | **916,858,953** | **523,704,575** |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | **22** | **1,010,740,473** | **916,858,953** |

Council has re categorize Development grant from investing activities to operating activities in financial year 2019/20

Hon. Bosco S. Mwanginde
Council Chairperson
Date: 28.9.2021

Tamimu Kambona
Council Director
Date: 28.9.2021

MWENYEKITI WA HALMASHAURI CHUNYA

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR CHUNYA DISTRICT COUNCIL

## STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2021

| | Notes | 2021 TZS ' | 2020 TZS ' |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Taxes and levies | 9 | 2,532,156,229 | 2,236,321,164 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 1,220,929,945 | 1,419,895,649 |
| Amortization of revenue grants | 11 | 15,879,844,681 | 15,429,327,444 |
| Revenue from exchange transactions | 12 | 154,057,650 | 64,844,959 |
| Fair value gains on investment | 13 | 7,398,750 | 1,726,375 |
| Amortization of capital grant | 30 | 2,365,071,420 | 491,428,156 |
| Other revenue | 14 | 362,387,500 | 120,366,000 |
| | | **22,521,846,175** | **19,763,909,747** |
| **Expenses** | | | |
| Provision for Loss | 16 | 32,769,324 | 218,478,499 |
| Wages, salaries and employee benefits | 17 | 13,079,771,960 | 13,342,004,488 |
| Supplies and consumables used | 18 | 3,774,073,603 | 4,190,193,519 |
| Maintenance expenses | 19 | 727,123,872 | 647,654,753 |
| Grants and other transfer payments | 20 | 519,445,980 | 381,013,861 |
| Finance Costs | 30 | 4,183,892 | 13,946,305 |
| Depreciation of property, plant and equipment | 25 | 422,582,717 | 460,897,797 |
| | | **18,559,951,347** | **19,254,189,222** |
| Share of associates surplus | | - | - |
| **Surplus during the year** | | **3,961,894,828** | **509,720,525** |
| **Attributable to:** | | | |
| Owners | | - | - |
| Non-controlling interests | | - | - |
| | | **3,961,894,828** | **509,720,525** |

Hon. Bosco S. Mwanginde
Council Chairperson
Date: 28.9.2021

Tamimu Kambona
Council Director
Date: 28.9.2021

## REPORT ON THE AUDIT OF FINANCIAL STATEMENTS

**Opinion**

I have audited the financial statements of Chunya District Council, which comprise the statement of financial position as at 30 June 2021, the statement of financial performance, statement of changes in net assets, cash flow statement and the statement of comparison of budget and actual amounts for the year ended, as well as the notes to the financial statements, including a summary of significant accounting policies.

In my opinion, the accompanying financial statements present fairly in all material respect, the financial position of Chunya District Council as at 30 June 2021, its statement of financial performance and cash flow statement for the year then ended in accordance with international Public Sector Accounting Standard (IPSAS) accrual basis of accounting and the manner required by the Local Government Finance Act Cap 290 (R.E.2019)

**Basis for Opinion**

I Conducted my audit in accordance with the International standards of Supreme Audit Institutions (ISSAIs). My responsibilities under those standards are further described in the auditor's Responsibilities for the audit of the financial statements section of my report. I am independent of Chunya District Council in accordance with the International Ethics Standards Board for Accountants' Code of Ethics for Professional Accountants (IESBA Code) together with the National Board of Accountants and Auditors (NBAA) Codes of Ethics, and I have fulfilled my other ethical responsibilities in accordance with these requirement.

I believe that the audit evidence I have obtained is sufficient and appropriate to provide a basis for my opinion.
Compliance with the Public Procurement Laws in Tanzania

**Subject Matter: Compliance audit on procurement of works, goods and services**

I performance a compliance audit on procurement of works, goods and services at Chunya District Council for the financial year 2020/21 as per the Public Procurement laws in Tanzania.

**Conclusion**

Based on the audit work performance, I state that, except for the matter described below, procurement of works, goods and services of Chunya District Council is generally in compliance with the requirement of the Public Procurement laws in Tanzania.

**Procurement of building materials out of TANePS system TZS. 271,316,405**

The Council procured building materials worth TZS. 271,316,405 out of TANePs system contrary to Reg. 342 of the Public Procurement Regulations, 2013 and Circular No.4 with reference No. EB/AG/485/01/Vol.xii/26 issued on 23 October 2019 by the Ministry of Finance which reminded all Accounting Officers to use TANePs.

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General,
Dodoma, United Republic of Tanzania.
March, 2022

217012401

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madai ya kukosa nyumba wananchi Magomeni Kota yashughulikiwe kwa amani

**KATIKA** gazeti la Nipashe toleo la jana, kulikuwa na habari kwamba wananchi 21 wanaodai kuwa wakazi halali wa nyumba za Magomeni Kota mkoani Dar es Salaam, wameulalamikia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuwa imewanyima nyumba wakati wana mikataba halali ya ukazi.

Licha ya kudai kukosa haki hiyo kama wenzao waliokuwa wameondolewa kupisha ujenzi wa nyumba mpya na kuleta mwonekano mzuri eneo hilo, wananchi hao wamedai kuwa TBA imewataka kama hawajaridhika waende mahakamani.

Kwa mujibu wa wananchi hao, baada ya kubaini kuwapo kwa tatizo hilo, walifuata hatua kuwasilisha kilio chao ikiwamo kwenda Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni na TBA.

Awali, walibainisha kuwa wapangaji waliokuwa na malalamiko ya kutorejeshwa katika nyumba hizo walikuwa 44 lakini baada ya mchakato wa utatuzi walibaki 21 ambao ndio wameambiwa waende mahakamani kama wanaona hawajaridhika.

Pamoja na kauli hiyo ya TBA, taarifa ambayo wanadai waliipata kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni iliwahakikishia kuwa mgogoro umemalizika na kwamba watakabidhiwa nyaraka lakini wakashangaa kuona kuwa baadhi ya watu waliopewa hawakuwa wapangaji katika nyumba za awali ambazo zilibomolewa.

Jambo hilo limechukua mlolongo mrefu tangu wakati wa ubomoaji wa nyumba za kota zilizokuwa katika mwonekano wa kizamani kwani wapangaji hao waliwahi kuwa katika mvutano na serikali na hatimaye kuahidiwa kwamba watarejeshwa baada ya kujengwa nyumba za ghorofa ambazo zimebadilisha mandhari ya eneo hilo.

Ni muhimu jambo hilo likapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili kuleta amani na maelewano na wananchi hao ambao wengi waliishi miaka nenda rudi, wapatiwe haki kama ilivyokuwa kwa wenzao ambao wamepewa nyaraka na kuwa wapangaji, wakiendelea kufurahia ukaribu wao uliodumu kwa miaka mingi.

Pamoja na TBA kutoa kauli kwamba wanaolalamika si wapangaji, jambo la kujiuliza ni kwa nini waliwapa nyaraka za kurejea kwenye nyumba hizo ilhali hawakuwa wapangaji? Hapo kuna jambo ambalo limejificha linahitaji uwajibikaji kwa waliotoa kauli hiyo.


Ni imani yetu kwamba lengo la serikali katika kubadili mandhari ya eneo hilo ilikuwa njema kwani nyumba za awali, zilizokuwa zimepewa jina la 'mabehewa', zilikuwa na mwonekano wa kizamani na nyingi zilikuwa zimechakaa. Kwa mantiki hiyo, kujengwa upya kumeongeza thamani ya eneo pamoja na hadhi ya wananchi wanaoishi hapo, hivyo haki itendeke.

Kama alivyosema mwanasheria wa wananchi hao kuwa hawafikirii kwenda mahakamani bali watatumia njia za mazungumzo, ni vyema pande husika zikakutana na kujadiliana na hatimaye kumaliza suala hilo ambalo linaanza kutia doa mpango wa serikali.

Ni dhahiri kwamba kuna harufu ya ujanja unjana katika mgawo wa nyumba hizo, hivyo mamlaka za serikali zinapaswa kutolinyamazia suala hilo. Mamlaka zilizopewa dhamana ya kuisimamia haki na kuchunguza vitendo vyovyote vilivyo kinyume cha haki, ziingilie kati ili kupata ukweli wa suala zima na kama kuna watu wanatumia nafasi zao kwa manufaa binafsi, wachukuliwe hatua.

Katika serikali, kuna mifumo mbalimbali ya kiuongozi hivyo kuanzia ngazi ya wilaya, kwa maana ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni hadi serikali kuu kwa maana ya wizara zenye dhamana ya ardhi na majengo, ziingilie kati na hatimaye kumaliza mgogoro huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuruhusu bidhaa hafifu kunavyoongeza umaskini

Na Mwandishi Wetu

**BIDHAA** hizi zinazofanana na zenye viwango zinazopatikana maeneo mbalimbali na zinatumika, lakini zinaponunuliwa hazidumu kama ni mabati hupauka rangi kwa muda mfupi na pia hutoboka kutokana na kutu.

Vipo vifaa vingine vya ujenzi vinavyopatikana kwenye soko lakini, unaponunua unaelezwa kuwa havina 'ubora, vina hitilafu'. Cha kushangaza vina chapa ya kibiashara, tena halali na inayomilikiwa na wazalishaji wanaofahamika.

Bidhaa hizo ambazo si imara zinalingana kivipimo kwenye utengenezaji na hazizalishwi kinyume cha sheria na wazalishaji au wauzaji hulipa kodi. Lakini kwanini visiwe na ubora? Unajiuliza.

Mathalani, kuna baadhi ya bidhaa za ujenzi zinazotumiwa utasikia mafundi wanatahadharisha hiyo ni 'masika moja kwisha habari', wakimaanisha hizo hazidumu muda mrefu, zinapoteza ubora na mvuto kwa kipindi kifupi zitakuwa zimechakaa.

Unapoziulizia bidhaa hizo madukani unaambiwa 'bei duni' au ya ghali hutolewa kulingana na ubora na kwamba zipo zinazopatikana kwa bei nafuu na zenye ubora hafifu licha ya kwamba zina vibali vya mamlaka zinazodhibiti ubora.

Maelezo zaidi yanayopatikana ni kwamba bidhaa za bei kubwa zinawahusu wenye kipato cha juu lakini, za bei ndogo zenye viwango vya chini ni za wateja wenye kipato kidogo.

Mambo haya yanayojiri kwenye ununuzi wa vifaa vya nyumbani kuanzia vyombo vya jikoni vya plastiki, bati hadi kioo. Kadhalika, simu na vifaa vya kielektroniki. Nguo nazo kuna madaraja zipo za hali ya chini zilizochujuka, kupauka na hata kutatuka.

Zinaelezwa kuwa zinaruhusiwa kuuzwa kulingana na wateja na mahitaji ya kila mmoja yanapatikana kulingana na fedha alizo nazo.

Inawezekana ni jambo la kushangaza, lakini ukweli ni kwamba bidhaa za bei ndogo halafu duni zinaongeza gharama za maisha kwa vile wateja watakuwa wananunua kila wakati kutokana na kuchakaa na kumalizika tena watazidi kupata hasara.

Mathalani, ukinunua mabati ya bei rahisi utayatumia kwa muda mfupi na yataanza kupauka na kuliwa na kutu, hivyo licha ya kuwa na kipato kidogo hujapata unafuu kwa sababu utagharamika tena kukarabati na kununua vifaa vingine zaidi tena kwa gharama kubwa.

Kadhalika, vifaa vya nyumbani kama vyombo vya plastiki hupasuka kwa muda mfupi na kumlazimisha ambaye mamlaka zinasema kipato chake ni kidogo, apate bidhaa zenye 'ubora unaostahili' kwa gharama nafuu bila kufahamu kuwa wanamuongezea gharama ya kununua mahitaji kila wakati.

Licha ya kwamba, pengine ni utaratibu unaokubalika kuwepo kwa madaraja ya bidhaa lakini suala la viwango na ubora ni la muhimu kwa sababu kuruhusu wafanyabiashara kuuza vitu duni ni kuligeuza taifa kuwa dampo , kuongeza umaskini miongoni mwa watu wa kipato cha chini ambao walitarajiwa kupata msaada zaidi.

Suala la kuuza bidhaa zisizo na ubora linaelekea kuwa la kawaida kwa vile hata kwenye viwanda vya kutengeneza matofali yanapangwa madaraja ya yaliyotengenezwa kwa sementi kidogo, mchanga wenye udongo na taka nyingi lakini pia yasiyomwagiwa maji ya kutosha.

Madaraja yapo kwenye vitu vingi lakini bila kubadilika na kuhoji hasara itakayopatikana kutokana na kuruhusu kutumia vitu vibovu mfano ujenzi wa nyumba mbovu za matofali duni, taifa haliwezi kuondokana na umaskini.

Kwa namna yoyote ile nyumba zitakazojengwa kwa matofali mabovu ya kiwango duni zitaleta athari kubwa kwa familia nyingi ambazo zitaendelea kuumia na kuishi ndani ya nyumba mbovu zinazovuja, zenye nyufa au kukosa makazi kwa sababu zinaweza pia kuanguka kutokana na kushindwa kuzikarabati.

Lakini, ugumu wa maisha utazidi kuwaumiza kutokana na kulazimika kujenga upya au kukarabati nyumba zao kwa vile kilichotumiwa kujenga kilikuwa hafifu. Yote hayo, yanafanyika kwa sababu ya kuruhusu bidhaa duni zinazoelezwa kuwa zina 'viwango' kuendelea kuuzwa .

Hali hiyo ni mpaka lini? Kuna haja ya kutazama upya kwa kuwa athari za kuruhusu bidhaa hafifu zipo na huenda zikaendelea kuishi na Watanzania hasa wasio na kipato kikubwa.

## HABARI KITAIFA

# PM aenda Tunisia Mkutano Wakuu wa Nchi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameondoka jana kuelekea nchini Tunisia, kumwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, katika Mkutano wa Nane wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa TICAD.

Mkutano huo utakaofanyika kwa siku mbili kuanzia leo, unatoa fursa ya kupanga mikakati ya ushirikiano na ajenda za kimaendeleo zitakazotekelezwa kati ya Japan na Afrika.

Tanzania imekuwa ikishiriki mikutano hiyo tangu kuanzishwa kwake mwaka 1993. Kutokana na mahusiano mazuri kati yake na Japan hususani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA), nchi imekuwa ikinufaika na utekelezaji wa miradi mbalimbali katika sekta za miundombinu ya barabara, nishati ya umeme, maji, elimu, afya na kilimo.

Kwa upande wa Afrika, mkutano huo unafanyika kwa mara ya pili baada ya wa mwaka 2016 uliofanyika jijini Nairobi, Kenya.

Kupitia mkutano wa saba uliofanyika Yokohama, Japan mwaka 2019, Japan ilitenga Dola za Marekani bilioni 20 kwa ajili ya kufanikisha malengo mbalimbali ya kimaendeleo kwa kipindi cha miaka mitatu (2019-2022).



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Morogoro, (MORUWASA) Mhandisi Tamimu Katakweba (kulia), akizungumza na Katibu Mwenezi wa CCM Kata ya Mindu, Christina Adamu, kuhusu mradi wa ukarabati wa miundombinu ya maji wa Kasanga, mkoani Morogoro juzi, eneo lilipo tangi la kuhifadhi maji lenye ujazo wa lita 135,000. **PICHA: IDDA MUSHI**

# MOI yatibu wagonjwa 1,500 mkoani Lindi

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu (MOI) imetoa tiba ya upasuaji kwa wagonjwa 1,500 katika Hospitali ya Nyangao mkoani Lindi katika kipindi cha miaka mitatu.

Kupitia huduma hiyo, serikali imeokoa Sh. bilioni 2.7 ambazo zingetumika kusafirisha wagonjwa wa mikoa ya kusini kufuata matibabu jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, akizungumza na waandishi wa habari wilayani humo jana, alisema taasisi ya MOI itaendelea kusogeza huduma zake karibu na wananchi.

Alisema hivi karibuni huduma za kibingwa za mifupa za MOI zitaanza kutolewa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini Mtwara.

"Tunashirikiana na wenzetu wa KCMC katika huduma za ubongo na mishipa ya fahamu, tunashirikiana na wenzetu wa Bugando katika huduma za upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu, tunashirikiana na wenzetu wa Benjamin Mkapa katika upasuaji wa nyonga na magoti, lengo letu ni kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi huko waliko kama serikali inavyoelekeza," alisema Dk. Boniface.

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, aliishukuru serikali kwa kuwajali wananchi wa mikoa ya kusini kwa kuwasogezea huduma za kibingwa za mifupa na kuwaondolea adha ya kuzifuata huduma hizo MOI.

"Ninaomba nianze kwa kuishukuru Wizara ya Afya kwa kazi kubwa, pia kwa namna ya pekee ninaomba niishukuru MOI ikiongozwa na Dk. Boniface, kwa kutekeleza kwa vitendo agizo la serikali la kusogeza huduma za kibingwa kwa wananchi hususani katika mkoa wetu wa Lindi na kuwapunguzia gharama wananchi, jambo hili limewajengea imani kubwa wananchi kwa serikali," alisema Ndemanga.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama, George Mbilinyi, alisema kuwapo kwa huduma za kibingwa za mifupa za MOI katika hospitali ya Nyangao, kumepelekea wagonjwa kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na mataifa jirani ya Msumbiji, Comoro na Malawi kufika hospitalini huko ili kupata huduma.

Akitoa shukrani kwa niaba ya uongozi wa Hospitali ya Nyangao, Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mtama, Dk. Dismas Masulubu, aliishukuru MOI kwa kuanzisha ushirikiano na hospitali hiyo na wagonjwa wamekuwa wakipata huduma za kibingwa bila kulazimika kuzifuata Dar es Salaam.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI**
**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI**

**TANGAZO LA KOZI YA UKARABATI NA MATENGENEZO YA BARABARA KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA STAHIKI YA NGUVU KAZI 'LBT'**

**1. UTANGULIZI:**
Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi "Institute of Construction Technology (ICoT)" ni Chuo cha Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi chenye makao yake makuu Morogoro. Chuo kinawatangazia wananchi wote kuwa kinatarajia kuendesha kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Udongo/Changarawe na Kozi ya lami kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Kampasi ya ICoT - Mbeya na ICoT – Morogoro kama ifuatavyo: -

| | Jina la kozi | Muda wa Mafunzo | Mafunzo yatafanyika |
|---|---|---|---|
| 1 | Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi | **Wiki Nne (4)** 12/09/2022 - 08/10/2022 | **Mkoani Morogoro (ICoT – Morogoro)** |
| 2 | Kozi ya Ukarabati na Matengenzo ya barabara za changarawe/udongo (Gravel/Earth Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. | **Wiki kumi (10)** 10/10/2022 – 17/12/2022 | **Mkoani Mbeya (ICoT – Mbeya)** |

**2. MASOMO YATAKAYOFUNDISHWA:**

(a) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:

Kozi hii, Washiriki watajifunza mada mbalimbali juu ya ujenzi wa barabara za lami (Surface Dressing for low Traffic Volume Roads) kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni: Maada juu ya vifaa na Mitambo midogomidogo, Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na matengenezo ya barabara za lami.

(b) Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya Barabara za Changarawe/Udongo (Gravel/Earth Roads) kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi:

Kozi hii, Washiriki watajifunza maada mbali mbali juu ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi pamoja na maada shirikishi ambazo ni; utaratibu wa kufungua kampuni, utaratibu wa kujaza kitabu cha zabuni, Teknolojia ya Udongo na Zege Ukarabati na Matengenezo ya barabara na Usimamizi sehemu ya kazi. Kipekee, kozi hii imelenga kumwezesha mshiriki kupata ujuzi wa kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Recurrent Maintenance'.

**3. NJIA ZA UFUNDISHAJI**
Mafunzo yatafanyika katika awamu mbili; awamu ya kwanza itakuwa nadharia (Darasani) na awamu ya pili itakuwa ni mafunzo ya vitendo ('Site').

**4. MALENGO YA KOZI**
Masomo katika kozi hizi yamelenga kumpatia mshiriki mbinu mbali mbali juu ya matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika:

i. Kufanya na kusimamia kazi za matengenezo ya barabara hasa matengenezo ya kawaida yaani 'Routine/Reccurent, Periodic and Emergency maintenance';
ii. Kufanya na kusimamia kazi za ukarabati wa barabara yaani 'road rehabilitation';
iii. Kuendesha na kusimamia miradi ya matengenezo na ukarabati wa barabara za vumbi/changarawe na barabara za lami;
iv. Kwa wajasiriamali, masomo haya yatawawezesha kujiajiri kwa kufungua kampuni za ujenzi wa barabara zinazotumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi yaani "SPECIALIST CIVIL WORKS-LABOUR BASED CONTRACTORING FIRMS" kisha kupata sifa za kisheria za kununua kazi za miradi ya ujenzi au ukarabati wa barabara zinazotolewa na TARURA au TANROADS.

**5. WALENGWA WA MAFUNZO:**

a) Wahandisi wote wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
b) Mafundi Sanifu wa barabara kutoka sekta ya Umma na binafsi,
c) Wasimamizi wa Miundombinu (Estates Managers) toka taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi,
d) Makandarasi wenye nia ya kujenga au kuimarisha uwezo wa kazi zao za matengenezo/ ukarabati wa barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi na,
e) Watu binafsi wenye uzoefu katika kazi za barabara au majengo na wanaohitaji kujiendeleza na kujifunza zaidi kazi za barabara.

**6. LUGHA YA MAFUNZO:**
Lugha itakayo tumika katika Kozi ya Lami kwa Kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi ambayo itaendeshwa kwa muda wa wiki nne (4) ni Kiingereza; kozi ya ukarabati na matengenezo ya barabara ya changarawe/udongo itaendeshwa kwa lugha ya Kiingereza.

**7. ADA ZA USHIRIKI**

a) Kozi ya Lami (Surface Dressing for Low Traffic Volume Roads)
   i. Mshiriki atapata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,000,000.00

b) Kozi ya Ukarabati na Matengenezo ya barabara za changarawe/udongo
   i. Mshiriki atakaye jitegemea huduma za chakula na malazi, atalipa ada kiasi cha Tsh. 800,000.00; na
   ii. Mshiriki atakayepata huduma za chakula na malazi zinazotolewa na Chuo atalipa ada kiasi cha Tsh. 1,600,000.00

Ada ya ushiriki zilipwe kwa kutumia 'Control Number' itakayotolewa kwa mtu atakayehitaji mafunzo kwa kuwasiliana na uongozi mapema kabla ya kozi kuanza. Inashauriwa kuwa ada ilipwe angalau wiki mbili kabla ya kozi kuanza.

**8. NAMNA YA KUTUMA MAOMBI YA KOZI:**

Wale wote watakao hitaji kujiunga na kozi yoyote kati ya hizi zilizotajwa hapo juu wanatakiwa kutuma maombi yao kwa kutumia anuani ya Posta au barua pepe zilizotolewa hapa chini au wanaweza kupiga simu kwa kutumia namba zilizotolewa kwa kupata maelezo zaidi.

**WASILIANA NASI**
**MKUU WA CHUO**

**TAASISI YA TEKNOLOJIA YA UJENZI ICoT,**

**S.L.P 963,**
**MOROGORO.**
**Simu : 023- 2935229/023- 2935226**
**: 0762 409087/0787059555/0786 384 062**
**Nukushi : 023-2935227**
**Barua pepe : mwti@morogoro.net**

**S.L.P 1957,**
**MBEYA.**
**Simu : 025 295 7484/5**
**: 0764775354/0769317404**
**Nukushi : 025 295 7486**
**Barua pepe : attimbeya@mow.go.tz, attimbeyafrica@gmail.com**

217012502

# TBL mlipakodi mkubwa, yaipa serikali mabilioni

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Bia Tanzania (TBL), imetambulika kama mlipajikodi mkubwa zaidi nchini baada ya kuchangia bajeti ya serikali kupitia mapato ya Sh. bilioni 472, mwaka 2021.

Malipo hayo ni pamoja na kodi ya mapato, kodi ya uhuru wa stempu na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Mwenyekiti wa Bodi ya TBL, Leonard Mususa, alibainisha hayo kwenye mkutano mkuu wa 49 wa wanahisa wa TBL uliofanyika Dar es Salaam.

Alisema, mapato ya kampuni yaliongezeka kwa asilimia sita kutokana na ongezeko la mauzo ya vinywaji vya bia na vinywaji vikali, asilimia 5.7 kwa bia, na asilimia tatu kwa vinywaji vikali. Alisema, kampuni iliendelea kutumia mkakati wa kibiashara kwa kuimarisha mwonekano wa chapa za vinywaji, matangazo kwa kutumia majukwaa mbalimbali ya vyombo vya habari na kutumia mkakati wa ubunifu wa kuhakikisha chapa pendwa za vinywaji vinavyozalishwa na kampuni vinapatikana katika vifungashio ambavyo wateja wanaweza kumudu kuvinunua.

"Matokeo yake, faida yetu ya uendeshaji katika kipindi hiki ilikuwa Sh. bilioni 179 na faida iliyopatikana baada ya kulipa kodi ilikuwa Sh. bilioni 134.

"Tuliidhinisha malipo ya gawio Sh. bilioni 75 kwa waheshimiwa wanahisa wetu, sawa na Sh. 255, kwa kila hisa ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia 60 ukulinganisha na mwaka uliotangulia," alibainisha. Mususa, aliongeza kuwa TBL Group inaendelea kutekeleza mkakati wa kustawisha jamii katika maeneo tunayofanyia biashara zetu.

"Biashara zetu haziwezi kuwapo bila wakulima, majisafi, jamii zenye afya, wazabuni wakubwa, watu mbalilmbali pamoja na wafanyakazi wetu na ustawi wa mfumo thabiti wa ikolojia.

"Mtazamo huu ndiyo msingi wa kila kitu tufanyacho. Kitengo chetu kinachoshughulika na mazingira ya kijamii na utawala (ESG), kinatekeleza jukumu kubwa kuhakikisha mkakati wa malengo ya kampuni yanafikiwa.

"Kupitia mkakati wa ushirikiano, TBL imewawezesha wakulima tunaofanya nao kazi kupata ujuzi, kuunganishwa pamoja na kuwezeshwa kifedha kwa lengo la kuwasaidia kuongeza uzalishaji na faida yao na matumizi mazuri ya maliasili.

"Tumedhamiria kufanikisha malengo endelevu ifikapo mwaka 2025 na kilimo bora ni moja ya malengo hayo. Tumedhamiria kuhakikisha kuwa asilimia 100, ya wakulima tunaofanya nao kazi katika mnyororo wetu wa kupata malighafi, wanapatiwa ujuzi, wanaunganishwa na kuwezeshwa kifedha hadi ifikapo mwaka 2025," alisema.

Alibainisha kuwa, biashara yao itaendelea kuwezesha wakulima wa ndani na kununua malighafi kutoka nchini, akisisitiza wamedhamiria kununua malighafi ya ndani ikiwa kama mdau mkubwa wa kukuza uchumi wa kijamii Tanzania.

Alisema kampuni imeendelea kufanikisha jukumu kubwa katika sekta ya kilimo ambapo katika kipindi cha mwaka uliopita, ilinunua asilimia 70 ya malighafi nchini ambayo ni shahiri, mahindi, mtama na zabibu kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa zake.

"Hivi karibuni serikali ilitoa kibali cha kuondolewa kodi ya asilimia 20 kwa shahiri itakayosindikwa nchini, hatua hii imewezesha kampuni yetu kuwekeza kwa kujenga kiwanda cha kusindika shahiri nchini.

"Hatua hii itawezesha kampuni kutumia shahiri iliyosindikwa nchini katika uzalishaji wa bidhaa zake za bia ifikapo mwaka 2027. Tutaendelea kushirikiana na serikali katika kufanikisha jitihada zake za mpango wa kujenga viwanda," aliahidi.

## Mama, mwanawe wasota rumande kesi ya mauaji

Na Grace Gurisha

MAMA na mwanawe wanaotuhumiwa kumuua ndugu yao Beatrice Magombola, wanaendelea kusota rumande kutokana na kutokamilika kwa upelelezi wa kesi hiyo.

Washtakiwa hao ni Alphonse Magombola (34), mkazi wa Bunju B Mpakani, na Sophia Mwenda (61), mkazi wa Mbagala, Dar es Salaam, ambao wameshtakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Beatrice na Alphonse ni mtu na mdogo wake na Mwenda ni mama yao mzazi. Tangu Machi 17, 2022 walikuwa mahabusu kwa ajili ya upelelezi hadi Julai 15, 2022, walipofikishwa mahakamani. Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga, wa Mahakama hiyo aliahirisha kesi hiyo jana hadi Septemba 8, 2022 kwa ajili ya kuangalia hatua ya upelelezi ulipofika.

Washtakiwa hao wapo mahabusu kutokana na mashtaka ya mauaji kutokuwa na dhamana kisheria. Awali, Wakili wa Serikali Faraja Ngukah, alidai washtakiwa hao wanatuhumiwa kwa shitaka moja la mauaji.

Alidai kuwa, washtakiwa hao wanatuhumiwa Desemba Mosi, 2020, wakiwa eneo la Kijichi ndani ya Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam, walimuua Beatrice Magombola.

TOL Gases Limited
We Deliver
Plot 4B, Nyerere Road, P.O Box 911, Dar es Salaam
Telephone: +255 22 2860047/9, Fax: 2 8 64041, E-mail: info@tolgases.co.tz

# DECLARATION OF DIVIDEND

The Board of Directors of TOL Gases Limited is delighted to announce that the Annual General Meeting of shareholders held on **19th August 2022**, approved the declaration of dividend of Tsh. 40.00 per issued and fully paid up shares for the year ended **31st December 2021.**

The following timetable for dividend payment;

| | |
|---|---|
| **Announcement of Dividend Payment:** | **19th August, 2022** |
| **Trading of Shares cum Dividend:** | **19th August 2022 – 9th September 2022** |
| **Trading of Shares Ex-Dividend:** | **10th September 2022** |
| **Closure of the Members Register:** | **14th September 2022** |
| **Re-Opening of the Register:** | **15th September 2022** |
| **Dividend Payment on/or about:** | **15th October 2022** |

Dividend will be paid directly to shareholders bank accounts.

**BY ORDER OF THE BOARD**

Directors: M.N.Shirima – Chairman(Tanzanian), S. Mponji – (Tanzanian), J.Massawe – (Tanzanian), S.Selestine – TR – URT (Tanzanian), Prof.ATemu – (Tanzanian), Eng. J. Machange – (Tanzanian) L.Kitoka – (Tanzanian)

217012802

# Kanisa Anglikana kupeleka wachungaji 600 na wenza wao kutalii Ngorongoro

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kutangaza sekta ya utalii ndani nje ya mipaka ya nchi, Kanisa Aglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika, limeandaa utaratibu wa kupeleka wachungaji pamoja na wenzi wao 600, kutembelea Hifadhi ya Ngorongoro.

Askofu wa Kanisa Aglikana Tanzania Dayosisi ya Central Tanganyika, Dk. Dickson Chilongani, alibainisha hayo katika hafla ya kuwaaga wake za wachungaji 111, ambao walisafiri jana kuelekea Ngorongoro kwa ajili ya kufanya utalii.

Alisema lengo la safari hiyo ni kuunga mkono jitihada za Rais Samia za kutangaza sekta ya utalii ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

"Dhumuni la safari hii ni kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan, kwa jitihada zake za kuitangaza nchi ndani na nje ya mipaka yetu kupitia filamu ya Royal Tour ili kuongeza idadi ya watalii kutoka nje na ndani," alisema Askofu Dk. Chilongani.

Alisema katika awamu ya kwanza jumla ya wake za wachungaji kutoka Dayosisi hiyo 111, wamesafiri jana kwenda Ngorongoro kutembelea hifadhi hiyo.

Kadhalika, alisema pamoja na kuunga mkono jitihada za serikali pia itawasaidia kwenda kupumzika na kurudi wakiwa na nguvu mpya ya kutekeleza majukumu yao.

"Hata katika vitabu vitakatifu vimeandikwa kuwa Mungu aliumba bustani ya Eden ambayo Adamu na Eva walikuwa wanakwenda kumpuzika na kuburudika hivyo hata wake hawa za wachungaji watapata fursa pia ya kupumzika na kumwomba Mungu ili wakirudi waje na nguvu mpya," alisema.

Alisema baada ya awamu hiyo ya kwanza kutakuwapo na kundi la pili na wenza wa wachungaji 100 na la tatu kwa idadi kama hiyo.

"Hadi kukamilisha safari zote tunatarajia kuwa wachungaji pamoja na wenza wao zaidi ya 600 watakuwa wamekwenda kutalii katika Hifadhi hii ya Ngorongoro Dayosisi yetu ndiyo kubwa kuliko zote kwa Kanisa Aglikana Duniani," alisema.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Shenyamule, akizungumza katika hafla hiyo alilipongeza kanisa hilo kwa kuanzisha utaratibu huo na kumuunga mkono Rais.

"Nipongeze sana kanisa kwa kazi nzuri ambazo mmeendelea kuzifanya kwanza kumtukuza Mungu na kushirikiana na serikali kuhudumia Watanzania," alisema Shenyamule.

Vilevile, alilipongeza kanisa hilo kwa kuwekeza katika elimu kwa kuwa na shule inayotoa elimu kwa mtaala wa kimataifa hali inayosaidia watu wa ngazi mbalimbali kuhamia Dodoma.

"Niwapongeze kwa kuwa na shule hii kwani kuna watu kama mabalozi ambao wanashindwa kuhamia hapa kutokana na kukosekana kwa shule za viwango vyao niwaahidi serikali itaendelea kuwapa ushirikiano muda wowote milango yetu itakuwa wazi,"alisisitiza.



Mtaalamu wa Macho, John Pastory (kulia), akimpima macho, Zulfa Rashidy wakati wa kambi maalum ya huduma ya upimaji wa afya ya siku tatu inayotolewa na Jumuiya ya Khoja Shia Ithnashar Tanzania kwa kushirikiana na taasisi za afya za serikali katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana waitwa kujiunga mafunzo JKT

**Na Faustine Feliciane**

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limetangaza nafasi za kujiunga na jeshi hilo kwa kujitolea kwa vijana wa Kitanzania wenye umri wa miaka kati ya 16 na 35 wenye elimu ya darasa la saba mpaka chuo kikuu.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi hilo, Meja Jenerali Rajabu Mabele jijiji Dar es Salaam, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema Mkuu wa Jeshi hilo ametoa wito kwa vijana wote wenye sifa kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kujitokeza kuchangamkia nafasi za mafunzo hayo.

"Utaratibu wa vijana kuomba na hatimaye kuchaguliwa kujiunga na mafunzo haya ya kujitolea utaratibiwa na ofisi za waheshimiwa wakuu wa mikoa na wilaya ambako mwombaji anaishi," alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Alisema, vijana na wananchi wote wanapaswa kufahamu kuwa jeshi hilo halitoi ajira kwa vijana, pia halihusiki kuwatafutia ajira katika asasi, vyombo vya ulinzi na usalama, taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali.

"Wapo watu ambao sio waaminifu wanatumia fursa hii vibaya kwa kutangaza JKT inatoa ajira, JKT haitoi ajira, ila kama fursa hiyo itatolewa basi vijana hawa na wengine ambao wakimaliza mafunzo haya wanawekwa kwenye Jeshi la akiba ndio watapewa nafasi," alisema.

Sifa nyingine wanaotakiwa kuomba nafasi hiyo ni lazima asiwe amepitia mafunzo mengine ya JKT kipindi cha nyuma wala kutumika Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo wala KMKM.

"Utaratibu wa kujiunga na JKT unaanza leo (Jana), wale watakaochaguliwa kujiunga watatakiwa kuripoti makambini Septemba na mafunzo tunatarajia yataanza Oktoba, yatakuwa ya miezi 24 na katika kipindi hicho, miezi minne itakuwa ya kujengwa ukakamavu na miezi 20 itakuwa ya stadi za maisha," alisema.

Alisema vifaa watakavyotakiwa kuwa navyo wakati wa kuripoti makambini vimeorodheshwa kwenye tovuti ya jeshi hilo.

# TRA yafikisha sita kortini kushindwa kusajili VAT

**Na Idda Mushi,** KILOSA

MAMLAKA ya Mapato Nchini (TRA) Mkoa wa Morogoro, imewafikisha mahakamani watu sita kwa makosa matatu tofauti ikiwamo kushindwa kuomba kusajiliwa kwenye Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), kuwazuia maofisa wa mamlaka hiyo kufanya kazi yao na kushindwa kuendana na matakwa ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Washtakiwa hao ni Kibwana Kidinilo, Kitete Sugar, Clement Gwila na Mathias Mligwa, pamoja na Gajoki LTD na Green Line Brothers ambao hawakutokea mahakamani.

Walisomewa mashtaka yao na Mwendesha Mashtaka Mwandamizi wa Serikali, Cherubini Chuwa, mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Agnes Ringo, katika Mahakama ya Wilaya ya Kilosa, wakidaiwa kutenda makosa hayo Julai 26, mwaka huu kwa nyakati tofauti.

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa hao kwa nyakati tofauti wanadaiwa kushindwa kuomba kusajiliwa kwenye kodi ya VAT, kinyume na kifungu 28 cha Sheria ya Kodi ya VAT sura 148, ikisomwa pamoja na kifungu cha 90 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi namba 10 ya mwaka 2015 yenye marejeo hadi mwaka 2019.

Shtaka la pili ni kuwazuia maofisa wa TRA kufanya kazi yao kwa kukataa kwa makusudi kurejesha fomu za VAT walizopewa, kinyume na kifungu cha 85 (3) (I) cha sheria hiyo ya usimamizi wa kodi.

Katika shtaka la tatu walishindwa kuendana na matakwa ya Sheria ya Kodi kwa kitendo cha kutofika kwa hiari kusajiliwa kwenye Kodi ya VAT kinyume na kifungu cha 28 cha sheria hiyo, kikisomwa pamoja na kifungu cha 82 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi.

Washtakiwa wote wanne waliofikishwa mahakamani hapo walikana mashtaka na kuachiwa kwa dhamana yenye masharti ya kutakiwa kila mmoja kuwa na wadhamini wawili wenye mali zisizohamishika zenye thamani ya Sh. milioni 20.

Upelelezi wa shauri hilo umekamilika na limepangwa kufikishwa tena mahakamani hapo Agosti 31, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa na kupanga tarehe ya kuanza kusikiliza.

# Wajawazito walalamika kutozwa fedha kujifungua

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

BAADHI ya wajawazito wa vijiji vya Mtakateni, Mkarakate na Makurani wilayani Masasi mkoani Mtwara, wamelalamika kutozwa kati ya Sh. 15,000 hadi Sh. 20,000 kwa ajili ya kulipia huduma za afya ikiwamo kujifungua kwenye zahanati zilizoko kwenye vijiji vyao.

Wanawake hao walitoa malalamiko hayo jana mjini hapo kwenye mkutano wa hadhara wa Mbunge wa jimbo hilo, Geofrey Mwambe, uliofanyika katika Kijiji cha Mtakateni.

Walidai kuwa wanapokwenda kwenye zahanati ya kijiji chao kupata huduma za afya za kujifungua wahudumu wanatoza fedha jambo linalowashangaza.

Renfrida Sijaona, alisema mjamzito akitaka kujifungua lazima atozwe kati ya Sh. 15,000 hadi 20,000 ndiyo apatiwe huduma katika zahanati.

Vile vile, alidai lazima wawe na vifaa mbalimbali wanavyotakiwa kutoka navyo nyumbani kama ndoo ya maji, beseni na plastiki atakayotumia kutandika wakati wa kujifungua.

"Mbunge, hivi wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano tunapaswa kulipia huduma ya afya maana sisi tunajua serikali ilitoa maelekezo kuwa ni bure hawa wanaotutoza wameelekezwa na nani? Alihoji Sijaona.

Asha Bakari, mkazi wa Mkarakate aliiomba serikali kuingilia kati suala la wajawazito kutozwa fedha ili kupata huduma za afya ikiwamo kujifungua.

Kwa upande wake, Mwambe alisema serikali imeshatoa maelekezo ya kwamba wazee zaidi ya miaka 60 watoto na wajawazito watapatiwa huduma za afya bila ya malipo yoyote.

Alisema kama kuna mhudumu yeyote wa afya anawatoza wajawazito fedha kwa ajili ya kulipia huduma anakwenda kinyume na maelekezo ya serikali na anapaswa kuchukuliwa hatua.

"Hakuna utaratibu kwa wajawazito, wazee na watoto kulipia huduma za afya iwe kwenye zahanati au hospitali yoyote ya serikali huduma kwa makundi haya ni bure hivyo yeyote akibainika kumtoza mjamzito ni makosa," alisema Mwambe.

Akizungumza na gazeti hili ofisini kwake kuhusu malalamiko hayo, Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri Masasi, Dk. Salumu Gembe, alisema serikali haijatoa maelekezo yoyote wajawazito kulipia huduma za afya wanapotaka kujifungua.

Alisema ofisi yake itafuatilia jambo hilo kwa lengo la kufahamu zaidi malalamiko hayo na iwapo kuna mhudumu wa afya atakayetambulika kuwatoza wajawazito na watoto hela ili kupata huduma atachukuliwa hatua.




Mkazi wa Mtwara, Mohamed Hassan Jongo, akiwa mwenye furaha baada ya kupokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 10.9 mkoani humo jana, alizoshinda kutoka kwenye bahati nasibu ya Biko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Tumieni mifumo ya mitandao kutafuta ajira'

**Na Julieth Mkireri**

VIJANA nchini wameshauriwa kutumia mitandao ya kijamii na mifumo ya kidigitali kwa ajili ya kutafuta ajira.

Mkurugenzi wa taasisi isiyo ya kiserikali inayojishughulisha na utoaji wa elimu ya matumizi sahihi ya Kidigitali (DA4TI), Peter Mmbando, alisema hayo wakati wa kuwajengea uwezo vijana masuala ya usalama wa kidigitali mitandaoni.

Mmbando alisema wamefanya mafunzo hayo kwa vijana ili waende wakawe mabalozi kwa wengine na kuelimishana jinsi ya kuacha kutumia lugha chafu au za chuki kwenye mitandao na kutengeneza kampeni ambazo zinaweza zikaharibu maudhui ya kimtandao.

Alisema elimu hiyo kwa vijana itawasaidia kujua iwapo mitandao inachukua utu wa kibinadamu kutokana na dunia ilivyobadilika wanatakiwa kuelewa kuwa sio kila kitu ni cha kuweka kwenye mitandao.

Kadhalika, alisema wanatakiwa kulinda watoto na vijana wa kike na wa kiume hata wazee hasa katika masuala ya usalama wa kidigitali mitandaoni.

Mmbando alisema wamefanya mafunzo hayo kwa vijana ili waende wakawe mabalozi kwa wengine na kuelimishana jinsi ya kuacha kutumia lugha chafu au za chuki kwenye mitandao na kutengeneza kampeni ambazo zinaweza zikaharibu maudhui ya kimtandao.

Alisema elimu hiyo kwa vijana itawasaidia kujua iwapo mitandao inachukua utu wa kibinadamu kutokana na dunia ilivyobadilika wanatakiwa kuelewa kuwa sio kila kitu ni cha kuweka kwenye mitandao.

Kadhalika, alisema wanatakiwa kulinda watoto na vijana wa kike na wa kiume hata wazee hasa katika masuala ya matumizi ya mitandao fedha kwa sababu wizi mkubwa unafanyika kwa njia ya kimtandao.

"Jukumu letu kuleta hii elimu ya masuala ya mtandao ni kutokana na watu wengi kutokujua matumizi sahihi ya kimtandao na pia mada mbalimbali za kiuchumi kupitia mitandao wengi hawachukulii maanani maendeleo endelevu ya mtandao," alisema.

Ukizingatia derikali kipaumbele chake ni kutaka kuhakikisha shule zote na sehemu mbalimbali za nchi kufikia 2025 ziwe zimeunganishwa na intaneti watu wataunganishwa, lakini hawajui matumizi sahihi ya kimtandao na vijana hao wanatakiwa kwenda kuwa mabalozi na kuwaelimisha wenzao na kutumia mitandao kutengeneza ajira badala ya kuharibu," alisema.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, kwa kushirikiana na mashirika ya Tactical Tech na Afrinic wanatarajia kufikisha elimu hiyo kwa vijana zaidi ya 100,000 hadi kufikia 2025.

Mmoja wa wakufunzi katika mafunzo hayo, Michael Mwakalikamo, alisema makosa mengi yanayoripotiwa polisi ni ya wizi wa kimtandao, kuiba utambulisho na picha za utupu.

Pia amewakumbusha wananchi ambao picha zao za utupu zinawekwa kwenye mitandao watoe taarifa mapema ili hatua za kisheria zichukuliwe na kukomesha tabia hiyo kwa wahusika.

# Bil. 2.7/- zaokolewa kusafirisha wagonjwa

**Na Yasmine Protace**

SERIKALI imeokoa zaidi ya Sh. bilioni 2.7 ambazo zingetumika kuwasafirisha wagonjwa kutoka mikoa ya Kusini na kuwapeleka jijini Dar es Salaam kufuata huduma za kibingwa za upasuaji zinazotolewa Hospitali ya Muhimbili Taasisi ya Huduma za Mifupa (MOI).

Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shahibu Ndemanga, alisema hayo alipoishukuru serikali kwa kuwasogezea huduma za kibingwa na kuiwezesha serikali kuokoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kingetumika kuwasafirisha wagonjwa kwenda MOI kufuata huduma za kibingwa za mifupa.

"Wagonjwa zaidi ya 1,500 wamefanyiwa upasuaji na madaktari bingwa wa MOI katika Hospitali ya Nyangao, mkoani Lindi katika kipindi cha miaka mitatu toka ilipoingia mkataba wa ushirikiano na hospitali hii ili kusogeza huduma za kibingwa kwa wananchi wa mikoa ya Kusini," alisema.

Alisema kutokana na uwapo wa huduma za kibingwa za mifupa katika Hospitali ya Nyangao, serikali imeokoa Sh. bilioni 2.7 ambazo zingetumika kusafirisha wagonjwa hao kufuata matibabu Dar es Salaam.

Ndemanga aliishukuru serikali kwa kuwajali wananchi wa mikoa ya Kusini kwa kuwasogezea huduma za kibingwa za mifupa na kuwaondolea adha ya kuzifuata huduma hizo MOI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Mtama, George Mbilinyi, alisema uwapo wa huduma za kibingwa za mifupa katika hospitali ya Nyangao umesaidia wagonjwa kutoka mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na mataifa jirani ya Msumbiji, Comoro na Malawi kufika hospitalini hapo ili kupata huduma.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema Taasisi ya MOI itaendelea kusogeza huduma zake karibu na wananchi na hivi karibuni huduma za kibingwa za mifupa za MOI zitaanza kutolewa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini Mtwara.

"Tunashirikiana na wenzetu wa KCMC katika huduma za ubongo na mishipa ya fahamu, tunashirikiana na wenzetu wa Bugando katika huduma za upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu, tunashirikiana na wenzetu wa Benjamin Mkapa katika upasuaji wa nyonga na magoti lengo letu ni kuhakikisha huduma zinawafikia wananchi walipo kama serikali inavyoelekeza," alisema.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mtama, Dk. Dismas Masulubu, aliishukuru Taasisi ya MOI kwa kuanzisha ushirikiano na Hospitali ya Nyangao ambapo wagonjwa wanapata huduma za kibingwa bila kulazimika kuzifuata Dar es Salaam.



Ukurasa 14

China na Tanzania katika ushirikiano wa kiuchumi kwa maendeleo endelevu




Ukurasa 13

Tupongezane kwa sensa ya amani na utulivu ila...


# BUFE

IJUMAA AGOSTI 26, 2022

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




Ukurasa 12

VIFURUSHI VYA UTT-AMIS

## Silaha 'vyuma vinapobana,'mkwamo mdororo kiuchumi

BIASHARA

# ASA yawatangazia wakulima habari njema ya kumaliza uhaba wa mbegu

**Na Renatha Msungu**

WAKALA wa Usambazaji Mbegu (ASA) umejiwekea lengo la kuzalisha tani 600,000 za mbegu za aina mbalimbali ifikapo 2030 ikiwa ni mkakati wa taifa kujitosheleza kwa mbegu na kuimarisha kilimo ambacho ni chanzo cha malighafi viwandani na chakula kwa wananchi.

Mtendaji Mkuu wa ASA, Dk. Sophia Kashenge, anasema katika mahojiano na Nipashe, wakati wa kilele cha Maonyesho ya Wakulima na Wafugaji, Nanenane mkoani Mbeya.

Akifafanua zaidi, anasema ASA inayozalisha tani 100,000, inalenga kuwa ifikapo mwaka 2030 wakala utazalisha tani 600,000 ambazo ni mahitaji halisi ya Watanzania kwenye sekta ya mbegu.

Aidha, anaeleza kuwa wakala una mashamba takribani Tanzania nzima na pia umejizatiti kukabiliana na ukosefu au upungufu wa mbegu kwenye mikoa yote unaolenga kuwa na mbegu bora.

Pia anawataka wakulima wajiendae kupata huduma bora kila wakati.

"Tumeongeza uwekezaji kwenye mashamba haya, tumetoka kuwa nayo nane hivi sasa yako 16 ni hatua kubwa sana. Na yote lazima yapandwe mbegu ili kuondoa uhaba kwa wakulima," anasema Dk. Sophia.

"Kila kitu tunacho na tunafanya uzalishaji kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, za utafiti, ugunduzi na udhibiti wa ubora wa mbegu, ndiyo maana mbegu zetu ni bora zaidi na wakulima wakizitumia kwa maelekezo ya maofisa ugani na kilimo watazalisha kwa tija,"anasema Dk. Kashenge.

Anafafanua kuwa, wanasambaza mbegu takribani mikoa yote kwa kuwa kiuzalishaji ASA, wamejitosheleza kwa sababu ya uwepo wa mashamba hayo katika kanda katika mikoa tofauti.

Mtendaji Mkuu anampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuwekeza kwenye kilimo ambacho anasema ni jitihada kubwa hivyo watendaji nao wanafanya kazi ipasavyo ili kuhakikisha wanawatimizia wakulima haja yao ili kufanikisha jitihada za serikali katika uwekezaji wa kilimo.

Anaikaribisha sekta binafsi ili kusaidiana na ASA kwenye utatuzi wa changamoto za kilimo na kuinua wakulima.

"Tunafanya kazi na kampuni kadhaa binafsi ili kuwafikia wakulima na kutimiza malengo tuliyojiwekea." Anasema.

Aidha, anasema wakala umetumia maonyesho hayo ya kitaifa kuwaelimisha wakulima matumizi ya mbegu bora na kuwauzia kwa bei elekezi. "Tumesambaza mbegu nyingi za aina mbalimbali kwa wakulima kwa bei nafuu," anasema.

Wakati huo kukiwa na msongamano wa wakulima na heka heka ili kupishana katika banda la ASA kwa ajili ya kununua mbegu bora kutoka kwa wakala.

Dk. Sophia anasema ASA imefufua mashamba ya kuzalisha mbegu katika maeneo mbalimbali ambayo awali yalikuwa hayatumiki lakini hivi sasa yanalimwa ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora.

Mtendaji Mkuu wa ASA, anasema wakala una mashamba 16 kwenye kanda mbalimbali yaliyozungushiwa uzio ili kuepusha uvamizi na uharibifu.



Dk. Sophia Kashenge. **PICHA: MTANDAO**

"Tuko vizuri kwenye suala zima la mbegu na tunashirikiana vizuri na sekta binafsi kuhakikisha mbegu zinawafikia wakulima kwa wakati ili kuwahi msimu wa kilimo na mwaka huu tumejipanga kusambaza mbegu za kutosha kwa kushirikiana na sekta binafsi kwenye usambazaji,"anasema.

Anawaambia wakulima pamoja na Nanenane kufikia kilele waendelee kufuata na kupata mbegu bora kwa wakati kutoa ASA ili kuinua kilimo.

"Niwaahidi kuwa safari hii tunawahakikishia wakulima kuwa kila mmoja atapata mbegu kwa wakati, lengo ni kuwapa mbegu bora ambazo ni kwa ajili yao." Sisi taasisi ya serikali tunaunga mkono jitihada za Rais Samia katika uwekezaji kwenye sekta ya kilimo, ndiyo maana tuko mstari wa mbele katika usambazaji wa mbegu bora."

Akielezea majukumu ya taasisi hiyo, anasema ni kuzalisha, kusambaza na kuziboresha zaidi mbegu ili wakulima wasisumbuke kwenye kilimo.

Anasema ASA ni tofauti na sekta binafsi ni wanazalishaji mbegu aina zote zaidi ya 47 ili zipate kwa muda sahihi kwa wakulima.

Anaongeza kuwa katika Viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, wakati wa Nanenane waliwauzia wakulima mbegu kwa bei nafuu za msimu ujao wa kilimo.

"Hivi sasa tunafika Tanzania nzima na kusambaza mbegu katika mikoa yote hiyo bila tatizo. Nanenane tulisambaza zaidi ya tani 20 za mbegu kwa wakulima wa mikoa ya Arusha, Shinyanga, Simiyu, Njombe, Kigoma, Iringa, Tabora na Katavi," anasema akieleza kuwa ni mafanikio makubwa.

Lugano Amosi ni mkulima anayenunua mbegu kwenye maonyesho, akisema hatua hiyo imewarahisishia kusaka mbegu madukani.

Anapongeza juhudi za serikali kutokana na kuwekeza kwa kiasi kikubwa kwenye sekta ya kilimo na hasa taasisi zinazohusika kufanya kazi na kushirikiana na wakulima.

Amos anasema msimu huu wa kilimo wameamua kuanza mapema maandalizi kutokana na uhakika wa kupata mbegu bora kutoka ASA.

"Nawaomba wakulima wenzangu tubadilike tujipange kuhakikisha tunapata mbegu bora, tunalima kisasa kwani hivi sasa kilimo ni biashara wakulima hatupaswi kubaki nyuma wala kulalamikia umaskini. Serikali inatusaidia nasi tuwajibike," anahimiza Amos.

VIFURUSHI VYA UTT-AMIS

# Silaha ‘vyuma vinapobana,’ mkwamo mdororo kiuchumi

• Ni mifuko ya uwekezaji inayomgusa kila mmoja

**Na Frank Monyo**

MDODORO wa uchumi unaosababishwa na mengi vikiwamo vita vya Russia na Ukraine umesababisha wafanyabiashara na wajasiriamali wengi kubaki njiapanda. Wapo wanaokwama au wasiojua cha kufanya.

Kuna walioanguka zaidi kibiashara kwa kukosa elimu sahihi ya fedha au namna ya kukabili hasara katika uwekezaji licha ya kwamba wapo waliojiunga na biashara ilhali hawana elimu sahihi ya fedha au namna ya kukabili changamoto zake.

Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa Asasi ya UTT-AMIS, Rahim Mwanga, anasema mifuko ya uwekezaji ni njia mojawapo sahihi ya kupunguza hatari hizo.

Mwanga anaeleza: “Mwekezaji anahitaji njia sahihi za kupunguza hatari za uwekezaji, ili kuendelea kutunza mtaji na kupata faida za ushindani, utaalamu, gawio, uwazi, urahisi wa kuweka na kutoa fedha zake na gharama nafuu za uendeshaji, vyote vinapatikana UTT-AMIS.”

Chombo hicho kinachosimamiwa na Wizara ya Fedha kwa zaidi ya miaka 17 sasa, kinatoa fursa kuwekeza katika mifuko yake ya Umoja, Watoto, Hatifungani, Jikimu, Wekeza Maisha na Mfuko wa Ukwasi ili kutunza thamani ya fedha, kukuza mitaji na kupata gawio.

Mwishoni mwa mwaka jana, UTT-AMIS ilifanya mikutano mikuu ya mwaka ya mifuko yote ikijivunia mafanikio makubwa na kuibua pia changamoto ya UVIKO-19.

Mkurugenzi Mtendaji wa UTT-AMIS, Simion Migangala, anazungumzia mafanikio akisema Mfuko wa Umoja thamani ya kipande imeongezeka kwa Shilingi 104 hadi 740 sawa na faida ya asilimia 16.6 kwa mwaka ulioishia Juni 2021.

Anasema mfuko huo ni wa kwanza kuanzishwa mwaka 2005 na kwa miaka 16 mfululizo unafanya vizuri na kwamba unawalenga wawekezaji wenye lengo la muda mrefu na kati.

### FAIDA ZA UWEKEZAJI

Ofisa Masoko anaeleza namna UTT-AMIS inavyofanya kazi huku ikiacha faida lukuki kwa mwekezaji, akisema imepewa leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kukusanya amana za wawekezaji na kuziwekeza.

“Tukishapata fedha tunakwenda kuwekeza katika masoko ya fedha na mitaji kulingana na waraka wa toleo la mfuko. Faida inayopatikana inarejeshwa na kugawanywa kwa wawekezaji na sehemu ya uwekezaji wao katika mfuko ndiyo inafahamika kama kipande,” anafafanua.



Ofisa Mwandamizi wa Masoko na Uhusiano wa UTT-AMIS, Rahim Mwanga, akielezea faida za uwekezaji katika mifuko mbalimbali. **PICHA: ZOTE MAKTABA**

> **“Mfuko wa Hati Fungani umelipa gawio la Shilingi 1.0 kila mwezi sawa na Sh. 12.0 kwa muda wa mwaka mmoja.**

Masoko ya mitaji, ni fedha inayohusisha dhamana za uwekezaji zaidi ya mwaka mmoja: “Mfano kuna kuwekeza kwenye hisa ambazo zimeorodheshwa na Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE), pia kuwekeza kwenye hati fungani za kampuni na serikali za muda mrefu,” anasema.

“Mifuko ya uwekezaji inawezesha wawekezaji wadogo kupata fursa za kuwekeza kwenye masoko ya fedha na mitaji kwa viwango vidogo vya fedha tena mara kwa mara. Wanapata fursa ya kuwekeza kwenye dhamana, ambazo katika hali fulani mwekezaji mmoja mmoja inakuwa ni ngumu au ghali kupata dhamana hizo,” anasema Mwanga.

“Kampuni ya UTT-AMIS, imekuwa ikitoa elimu ya fedha mara kwa mara kwa makundi tofauti kuhusu faida na jinsi ya kuwekeza katika mifuko yao, kwa malengo ya muda mfupi na mrefu,” anasema Mwanga.

### MFUKO WA UMOJA

Anasema uko uwazi na wenye uwiano sawa wa uwekezaji, ukiufanya kuwa bora na wenye uwekezaji wa kiwango cha kati, aidha ni mfuko unaoruhusu kuwekeza kiwango kisichozidi asilimia 50 ya fedha zako kwenye hisa zilizoorodheshwa DSE na asilimia 50 nyingine zinawekezwa kwenye masoko mengine ya fedha na mitaji yenye sifa tofauti.

Sera ya uwekezaji kwa upande mmoja, ni mpango uliowekwa na mfuko kutawanya rasilimali zake. Pia ni mpango mkakati na kinga, endapo eneo moja la uwekezaji linaathirika.

Anauelezea kuwa ni uwekezaji wenye hisa ulio kwa kiwango cha chini, ikilinganishwa na eneo lenye mapato ya kudumu (fixed Income).

Mwanga anasema, thamani ya kipande kwa sasa imeongezeka kutoka Shilingi 104 na kufikia Sh. 740 kwa kila kipande, sawa na faida ya asilimia 16.6 kwa mwaka ulioishia Juni 2021.




Wananchi wakitembelea banda la UTT-AMIS wakati wa maonyesho ya Sabasaba, mwaka huu.

### MFUKO WA UKWASI

Anasema, madhumuni ya mfuko huo ni mpango unaotoa njia nyingine ya uwekezaji kwa wawekezaji wanaotaka kuweka fedha kwa kipindi cha muda mfupi na mrefu. Kukabili hatari na athari kidogo katika uwekezaji na ukwasi wa hali ya juu, ndilo dhumuni hasa la mfuko huu.

Anaieleza sera ya uwekezaji huo kuwa ni kiwango cha chini cha uwekezaji katika masoko ya fedha kitakuwa asilimia 50 na fedha inayobaki itawekezwa katika dhamana za serikali. Huo ni mfuko usiowekeza kwenye hisa.

“Chaguo la mpango wa Uwekezaji wa Mfuko huu linatoa fursa ya kukuza mtaji. Pia mwekezaji anaweza kutoa fedha zake wakati wowote bila gharama yoyote,” anafafanua.

Nani anaruhusiwa kuwekeza? Anasema mfuko uko wazi kwa Mtanzania aliye ndani au nje ya nchi, watu binafsi (ikijumuisha watoto), asasi, mifuko ya pensheni, benki, taasisi za serikali, vyombo vya ulinzi na usalama na mashirika mengine.

Mwanga anaeleza kuwa Mfuko wa Ukwasi, umeongezeka ukubwa kwa Shilingi bilioni 103.1 sawa na asilimia 91.4; kutoka bilioni 112.8 Juni 2020 hadi bilioni 215.9 Juni 30, 2021. Anaongeza, pia kuwa katika kipindi hicho hicho thamani ya kipande iliongezeka kwa Shilingi 37.5 sawa na faida ya asilimia 15.3 kwa mwaka.

“Faida ya Mfuko wa Ukwasi kwa kipindi cha mwaka mmoja ni asilimia 15.3 ikilinganishwa na faida ya asilimia 15.1 iliyorekodiwa mwaka uliopita 2020. Faida ya asilimia 15.3 ni tafsiri ya ongezeko kwenye mtaji wa mwekezaji kwa mwaka huo,” anasema Mkurugenzi Migangala.

### MFUKO WA WATOTO

Mwanga anaufafanua kuwa ni mpango ulio wazi kwa watoto unaokusudia kukuza mtaji kwa muda mrefu kupitia uwekezaji wa mseto kwa kuwekeza kwenye hisa zilizoorodheshwa kwenye soko la hisa na dhamana.

Umri wa mtoto wa kujiunga na mfuko, uwekezaji unafanywa kwa mtoto wa umri chini ya miaka 18 na anayeruhusiwa kuwekeza kwa Watanzania walio ndani na nje ya nchi, pia watu binafsi, kampuni, taasisi, benki na asasi za kiraia, huku uwekezaji ukitakuwa ufanywe kwa manufaa ya mtoto.

Anaeleza, kwa kipindi Juni, 2020 hadi Juni 30,2021 thamani ya kipande iliongezeka hadi kufikia Shilingi 455.2 kutoka 380.9 mwaka jana, akisema ukubwa wa mfuko huo ni Shilingi bilioni 4.2, ikilinganishwa na bilioni 3.5 Juni 30, 2020 ikiwa sawa na ongezeko la Shilingi milioni 700.

### MFUKO WA JIKIMU

Mwanga anasema lengo la Mfuko wa Jikimu ni kukuza na kutoa gawio kutokana na mapato ya ziada kwa vipindi tofauti, pia kumkuzia mwekezaji mtaji.

Anasema, mfuko unatoa fursa mbili za uwekezaji, mapato ya robo mwaka, pia mwaka mzima, kwa kuambatanisha na ukuaji wa vipande.

Kiwango cha chini cha uwekezaji katika mfuko huo kwa mpango wa mapato ya robo mwaka, unatajwa kuwa ni Shilingi 2,000,000 na milioni moja kwa mpango wa gawio kwa mwaka, pia Shilingi 5,000 kwa mpango wa ukuaji mtaji kwa mwaka.

“Kiwango cha chini cha uwekezaji wa nyongeza au unaofuata (additional investment) ni Sh.15,000 kwa mpango wowote wa gawio na Sh.5,000 kwa mpango wa ukuaji mtaji kwa mwaka, hakuna ukomo wa kiwango cha kuwekeza,” anafafanua.

Anataja faida nyinginezo katika Mfuko wa Jikimu kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2021 kuwa ni kulipa gawio lenye thamani ya Shilingi bilioni 1.2 sawa na Sh. 12 kwa kila kipande.

“Hadi kufikia Juni 30, 2021 rasilimali za mfuko zilifika Shilingi bilioni 17.9 ikilinganishwa na bilioni 17.6 mwaka uliopita,” anasema na kuongeza kuwa: “Faida ya Mfuko wa Jikimu iliendelea kuimarika na kuongezeka kutoka asilimia 15.6 katika mwaka wa fedha uliopita hadi asilimia 18.8 katika mwaka wa fedha ulioisha Juni 30, 2021.”

### HATI FUNGANI

Mwanga anaeleza kuwa Mfuko wa Hatifungani kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2021 faida ilikuwa asilimia 15.7 ikilinganishwa na asilimia 16.2 mwaka uliotangulia.

“Mfuko wa Hati Fungani umelipa gawio la Shilingi 1.0 kila mwezi sawa na Sh. 12.0 kwa muda wa mwaka mmoja,” anasema.

Mwanga anazungumzia Mfuko wa Wekeza Maisha, akisema una zaidi ya miaka 10 sasa, ukiambatanishwa na faida za bima, mwekezaji katika mfuko huo, ana lengo la kiasi anachotaka kuwekeza katika muda wa miaka 10, kiwango cha chini ni Shilingi 1,000,000. Ni hiari yake kuwekeza kwa mkupuo au awamu.

Mwanga anatoa mfano binafsi, baada ya miaka 10 alifungua kiwanda kidogo cha kutotoa mayai ya kuku na kuuza vifaranga na mayai, akifafanua: “Niliweza kununua mashine (incubator) kwa sasa kipato changu kimeongezeka sana.”


Mwanga anakumbusha ukubwa wa mfuko huo kwa sasa umeongezeka kwa Shilingi milioni 400 (ziada 28.6%) hadi bilioni 1.8 kutoka shilingi bilioni 1.4 mwaka 2020.

“Thamani ya kipande kwa muda wa mwaka mmoja ulioishia Juni 30, 2021 iliongezeka kwa shilingi 125.8 sawa na asilimia 25.6 hadi kufikia Shilingi 617.3 kwa kila mwaka,” anasema.

---

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Tupongezane sensa ya amani na utulivu ila...






**NA JOSEPH KULANGWA**
**+255 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

ASALAAM aleykum Watanzania. Bila shaka mwaendelea na sensa ya watu na makazi. Nishukuru kwa niaba ya wenzangu kwamba jambo hili limeenenda vizuri kwa utulivu mkubwa na amani. Nijuavyo kwa Watanzania huwa hapa haribiki jambo ambalo kwa hakika wanajua kuwa ndilo linaloweza kuwakwamua kutoka mkwamo wa maisha, mojawapo ni hili la sensa.

Karibu kila mmoja kupitia kampeni na mafunzo yaliyotolewa na hatimaye vitendo, wamejua sensa ni nini na inafanyikaje na kwa nini. Wamejua mwishowe ni mipango bora ya maendeleo.

Ni hakika Oktoba tutakuwa tunajua tuko wangapi kwa jinsia, rika na rangi nchini na hivyo pia kufahamu kuwa mkate au keki yetu ya taifa itagawanywaje kwa mujibu wa idadi.

Nimpongeze sana Chifu Hangaya kwa kuliongoza hili mpaka hapo tulipofikia, lakini wote waliomsaidia kuliongoza na kulisimamia mpaka hapa kwa taratibu nzuri.

Kwa kutambua umuhimu wa sensa, Chifu Hangaya akatangaza Agosti 23 iwe mapumziko, ili kaya zibaki majumbani kupokea wageni, makarani wa sensa na kuhojiwa ili kupata taarifa za ndani zaidi na kuzifanyia kazi.

Kama mjuavyo Wabongo, baadhi hiyo siku wakaona ndiyo ya kufanya mambo yao, wakaigeuza kuwa mapumziko kama Jumamosi na Jumapili, hao wakajitupa kunako viti virefu kumwagilia moyo na kuacha wengine wakihesabiwa.

Kwa waliokuwa watiifu wakidhani sensa ni siku moja, wakabaki majumbani bila kuona makarani kutwa nzima, akahanikiza malalamiko kuwa ni bora ingekuwa siku ya kazi tu wakaenda kuzalisha mali.

Walipata faraja walipomsikia Kamisaa Mkuu wa Sensa, Anne Makinda akiwambia hili jambo si la siku moja bali saba, hivyo hapana haja ya kuhamanika na kuzua mtafaruku usio na maana. Watu wakatulia wakijua kuna kesho na kesho kutwa.

Lakini sasa wengine wakahoji sababu ya Agosti 23 kuwa ya mapumziko, ilhali sensa si ya siku moja tena, kwamba inaendelea mpaka siku zisizo za mapumziko.

Ukifikiria, ni kweli, kwa sababu kama walikaa nyumbani na makarani wasitokee, ni nini maana yake?

Siku hiyo ilifanywa ya mapumziko kwa sababu sensa zilizopita zilikuwa ikifanywa Jumapili, lakini ikaonekana ni siku ya Ibada, hivyo kuingilia imani za watu, wakishindwa kujigawa kuhesabiwa na makarani au na Mungu!

Alhamdulilahi, inaonekana tunaelekea kumaliza salama u salmini, ingawa kuna mambo inabidi kuyatazama kwa siku zijazo, kwani siku zote ni vizuri kuboresha jambo lililopo kwa ajili ya mustakabali mwema zaidi.

Natamani siku Chifu Hangaya atakapokuwa anatangaza matokeo ya sensa, nimsikie pamoja na pongezi kwa kazi nzuri, akisema: “Nimesikiasikia vijilalamiko lalamiko hivi, kwenye vishikwambi na vijiposho vyenu makarani.

“Nadhani kuna kitu ingawa hakijawekwa hadharani, natarajia nitaambiwa, ili kama kuna ulazima basi nikutakeni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere na mwenzio wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU), Salum Hamduni.

“Hebu mkatazame huko kuna nini, ili haya yasijirudie tena miaka 10 ijayo.”

Nitatamani kumsikia kwa sababu ni kweli kuna vijilalamikolalamiko kuanzia kuajiri makarani, ununuzi wa vishikwambi na posho.

Mambo haya yanasemwasemwa chinichini huko, kwani panapofuka moshi hakika pana moto. Kama yapo kweli yajulikane, rangi za mama zionwe, ili miaka 10 ijayo kuwe na utaratibu unaoeleweka, kuanzia kupata makarani, vifaa na malipo yao.

Mathalan, ningekuwa mimi, ningejiuliza hivi ni kwa nini kuajiri makarani, wakati tuna viongozi wetu wa mashina anaotujua nje ndani, tunavyoishi, tunavyokula kuvaa na hata kulala. Wanajua hata kuku tulionao. Kwa nini wasitumike hawa kutuhesabu?

Viongozi wetu wa mitaa hizi ndizo ingekuwa kazi zao. Na kwa kweli hata hizo posho zingewapoza kidogo na kuonekana kuwa kweli wanatambuliwa kwa kazi zao zilizotukuka.

Hawa kwa kweli ndio wanajua shida za wananchi huku chini, kuliko kutafuta watu na kuwachukua kwa misingi ya upendeleo. Tuliona mahali chama fulani kikilazimisha vijana wao kuandikishwa makarani. Kila kizuri hakikosi kasoro. Tukaziondoshe basi hizi kadhia. Alamsiki!

UCHUMI

# China na Tanzania katika ushirikiano wa kiuchumi kwa maendeleo endelevu

Na Chen Mingjian




Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, akiongoza mkutano wa waratibu kuhusu utekelezaji wa hatua za ufuatiliaji wa Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC), uliofanyika kwa njia ya mtandao jijini Beijing, Agosti 18, 2022. **PICHA: XINHUA**

AGOSTI 18, mwaka huu, ulifanyika mkutano wa waratibu kuhusu utekelezaji wa matokeo ya mkutano wa nane wa mawaziri wa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) uliofanyika kwa njia ya mtandao. Mkutano huo uliongozwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa Senegal, nchi mwenyekiti mwenza wa Afrika wa FOCAC, wawakilishi wa kanda ndogo za Afrika, Kamisheni ya Umoja wa Afrika na wajumbe wa kidiplomasia wa nchi za Afrika nchini China.

Mkutano huo ulitathmini kwa kina maendeleo yaliyofikiwa katika utekelezaji wa matokeo ya mkutano wa nane wa mawaziri na kufikia makubaliano muhimu katika ufuatiliaji pamoja na kukuza zaidi urafiki na ushirikiano kati ya China na Afrika.

Aidha, mkutano huo ulipitisha kwa kauli moja Taarifa ya Pamoja ya Mkutano wa Waratibu kuhusu tekelezaji wa Vitendo vya Ufuatiliaji wa Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa FOCAC, na hivyo kutuma tena ishara za kuimarisha mshikamano na ushirikiano, kulenga maendeleo na matokeo ya ushindi wa pande zote na kusimamia haki na uadilifu.

Novemba, mwaka jana, mkutano wa nane wa mawaziri wa FOCAC ulifanyika kwa mafanikio huko Dakar na Rais Xi Jinping wa China alitangaza “programu tisa” za ushirikiano kati ya China na Afrika.

Katika mkutano wa waratibu, Waziri Wang Yi, kwa niaba ya China, alitoa taarifa kwa washiriki kuhusu maendeleo ya hivi karibuni katika utekelezaji wa mkutano wa nane wa mawaziri wa FOCAC, hususan “programu tisa”, akiwasilisha “ripoti ya shule” yenye alama bora kwa Wachina na Waafrika.

Kwa juhudi za pamoja za China na Afrika, utekelezaji wa matokeo ya mkutano wa nane wa mawaziri una mwanzo mzuri. Ushirikiano kati ya China na Afrika umehimili shinikizo la kudorora kwa uchumi wa dunia na kudumisha hali chanya na inayoboresha.

Katika nusu ya kwanza ya mwaka huu, biashara kati ya China na Afrika ilifikia Dola za Kimarekani bilioni 137.38 na kusajili ukuaji wa mwaka hadi mwaka wa asilimia 16.6. Uagizaji wa bidhaa za China kutoka Afrika katika kipindi hicho uliongezeka kwa asilimia 19.1 mwaka hadi mwaka.

Aidha, ndani ya miezi saba baada ya mkutano wa nane wa mawaziri, kampuni za China ziliwekeza dola za Kimarekani bilioni 2.17 barani Afrika na zaidi ya Dola bilioni mbili kati ya Dola bilioni 10 za fedha za biashara zilitengwa.

> **“ Novemba, mwaka jana, mkutano wa nane wa mawaziri wa FOCAC ulifanyika kwa mafanikio huko Dakar na Rais Xi Jinping wa China alitangaza “programu tisa” za ushirikiano kati ya China na Afrika.**

Mazao mengi ya kilimo ya Afrika yamefikia soko la China kupitia ‘green lanes’ na zaidi ya Dola bilioni tatu zimetolewa kati ya Dola bilioni 10 za mikopo zilizoahidiwa kwa taasisi za fedha za Afrika. Takriban Dola bilioni 2.5 za mikopo zilielekezwa kwenye programu za kipaumbele za Afrika.

### MAPAMBANO YA UVIKO-19

Pamoja na hayo, China imekuwa ikitekeleza kikamilifu ahadi zake za kuunga mkono juhudi za Afrika za kupambana na janga la UVIKO- 19. Ndani ya miezi saba baada ya mkutano wa nane wa mawaziri, China ilitoa dozi milioni 189 za chanjo kwa nchi 271 za Afrika.

Kwa sasa, uzalishaji wa pamoja wa chanjo barani Afrika una uwezo wa kila mwaka wa dozi zipatazo milioni 400. China kwa mara nyingine imethibitisha kwa vitendo na matokeo ya kweli kwamba ushirikiano kati ya China na Afrika ni wa vitendo, si “maneno”, kwamba China daima hutimiza maneno yake mbele ya ndugu wa Afrika na kwamba uungaji mkono wa China kwa maendeleo ya Afrika ni wa kudumu daima.

Ushirikiano wa China na Tanzania siku zote uko mstari wa mbele katika ushirikiano kati ya China na Afrika. China na Tanzania zinatilia maanani utekelezaji wa ‘programu tisa. Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania, Balozi Liberata Mulamula, wamekutana mara mbili. Ya kwanza ni ana kwa ana na ya pili kupitia kiunga cha video.

Agosti 19, mwaka huu, ulifanyika mkutano wa sita wa Kamati ya Pamoja ya Uchumi, Ufundi na Biashara ya China na Tanzania. Katika mkutano huo, pande hizo mbili zilijadiliana kina kuhusu utekelezaji wa ‘programu tisa’ na upanuzi wa maeneo ya ushirikiano.

### UKUAJI BIASHARA

Kuanzia Januari hadi Juni, mwaka huu, kiwango cha biashara kati ya China na Tanzania kilifikia Dola za Kimarekani bilioni 3.558 na kusajili ongezeko la mwaka hadi mwaka la asilimia 31.5.

Tanzania imetia saini hati ya kutotoza ushuru wa forodha kwa asilimia 98 ya bidhaa zake zinazouzwa nje ya nchi kwenda China na China itaondoa mkopo mmoja usio na riba kwa Tanzania ambao ulikuwa umefikia mwisho wa kulipwa mwishoni mwa mwaka 2021.

Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, iliyojengwa na fedha za Wachina, imezinduliwa. Kituo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi na Huduma cha Mkoa wa Kagera kilichofadhiliwa na China, ambacho ujenzi wake umekamilika, kitakabidhiwa hivi karibuni. Hivi sasa, China na Tanzania zinafanya mawasiliano ya karibu kuhusu ushirikiano wa teknolojia ya Juncao pamoja na miradi mingine midogo midogo ambayo itaboresha maisha ya watu wa Tanzania.

Aidha, ujenzi wa njia ya pili ya uzalishaji wa klinka ya Huaxin Maweni tani 4,000 kwa siku katika Mkoa wa Tanga, ambayo ni sehemu ya uwekezaji mkubwa zaidi wa China nchini Tanzania, tayari umeanza.

Awamu ya tano ya reli ya kisasa (SGR), Kituo cha Umeme wa Maji cha Julius Nyerere na miradi mingine mikubwa ya miundombinu inayofanywa na kampuni za Kichina inapiga hatua kwa kasi.

Maendeleo mapya yamepatikana katika mabadilishano ya watu kwa watu kati ya nchi zetu mbili, ambayo ni pamoja na kutiwa saini kwa Mpango wa Utekelezaji wa Miaka 2022-2025 chini ya Mkataba wa Utamaduni wa Serikali ya China na Tanzania na kurejesha safari za moja kwa moja kati ya Dar es Salaam na Guangzhou zinazoendeshwa na Shirika la Ndege la Tanzania (ATC).

Mafanikio haya yaliyopatikana kwa bidii ni matokeo yasiyoweza kuepukika ya ushirikiano wa dhati kati ya China na Tanzania, na yameongeza msukumo mkubwa katika kuimarisha zaidi urafiki kati ya nchi hizi mbili.

Katika kusonga mbele na kufanikisha azma hiyo, China itaendelea kuoanisha mahitaji na mikakati yake ya maendeleo na ya Tanzania, kushirikiana na upande wa Tanzania kusukuma mbele kwa uthabiti utekelezaji wa matokeo ya mkutano wa 8 wa mawaziri wa FOCAC, kukuza ushirikiano wa hali ya juu wa Ukanda na Njia, na kuendelea kuimarisha ushirikiano katika nyanja za kilimo, viwanda na ujenzi wa miundombinu.

China pia itapanua ushirikiano na Tanzania katika sekta zinazoibukia, kama vile uchumi wa kidijitali na uchumi wa kijani. Juhudi hizi zinalenga kuunga mkono jitihada za Tanzania za kuharakisha maendeleo yake huru na endelevu na kuchangia katika ujenzi wa jumuiya ya China na Afrika yenye mustakabali wa pamoja katika enzi mpya.

***Mwandishi ni Balozi wa China nchini Tanzania.***

## Mkakati waongeza uwezo jamii kukabiliana na maafa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI wa Idara ya Menejimenti ya Maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu amesema kuwapo kwa mkakati wa nchi wa kupunguza athari za maafa (2020-2025) umeongeza uwezo wa jamii kujiandaa na kukabiliana na maafa mbalimbali.

Meja Jenerali, Michael Mmanga alibainisha hayo jana jijini hapo alipofungua warsha ya kuandaa taarifa ya nchi ya utekelezaji wa mkakati wa kimataifa wa Sendai (2015-2030).

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika mapambano dhidi ya maafa ambayo hujitokeza katika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha athari.

"Nchi yetu imekuwa ikishuhudia kuongezeka kwa matukio ya majanga ambayo yamekuwa yakisababishwa na sababu mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabianchi na shughuli za kibinadamu," alisema.

Aliongeza kwamba pindi maafa yanapotokea, husababisha madhara mbalimbali ikiwamo vifo, majeruhi, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu ya umma iliyotumia gharama kubwa kujengwa.

"Kwa ujumla, majanga haya yamekuwa yakisababisha matokeo hasi katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kutokana na kupotea kwa mafanikio yaliyopatikana kwa muda mrefu na hivyo kuzorotesha hatua za maendeleo," alisema.

Mshauri Mkuu Afrika kutoka Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupunguza Hatari za Maafa (UNDRR), Hachim Badji, alipongeza serikali kwa kuendelea kuchukua hatua za kukabiliana na maafa na kushirikisha taasisi mbalimbali.

"Warsha hii itumike kama fursa ya kubadilishana taarifa, uzoefu, mafanikio ambayo tumeyapata tangu mwaka 2015 tuweze kujua wapi tulipotoka, tulipo na tunapoelekea katika mapambano haya, kama UNDRR tutatoa ushirikiano kufikia malengo yaliyowekwa," aliahidi.

Ofisa Mwandamizi Uratibu wa Maafa kutoka Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Juvenal Kisanga, alibainisha kuwa WFP imekuwa ikifanya kazi kwa kushirikiana na serikali kuhakikisha maafa yanadhibitiwa na wananchi kufanya shughuli zao katika mazingira salama.

"UN kupitia wanachama wake waliopo nchini, tunafanya kazi kwa kufuata vipaumbele vya serikali kwa sababu yenyewe inatengeneza sera, mikakati na mipango ya kupunguza athari za maafa na sisi tunaunga mkono ili kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao," alisema.

# Serikali yawaita wadau mapitio sera ya sayansi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka wadau kutoa maoni ya mapitio ya rasimu ya sera ya sayansi, teknolojia na ubunifu pamoja na kiunzi cha uratibu wa masuala ya ubunifu nchini.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Caroline Nombo, alitoa raia hiyo jana jijini hapo alipofungua kikao kazi cha wadau hao kilichoandaliwa na wizara hiyo, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Alisema lengo la mapitio ya rasimu hiyo ni kuwa na sera na mikakati inayoendana na kasi ya mabadiliko ulimwenguni na kukidhi mahitaji ya nyanja mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

"Mapitio ya sera ya mwaka 1996 yamebaini changamoto na mahitaji mbalimbali ambayo yamepelekea siyo tu kuhuisha sera iliyopo bali pia kuandaa kiunzi cha uratibu wa masuala ya ubunifu nchini," alisema.

Alieleza kuwa kiunzi hicho ni nyenzo itakayorahisisha utekelezaji wa sera pamoja na kuimarisha uratibu na usimamizi wa ubunifu katika ngazi mbalimbali nchini.

"Ni matumaini yangu mtashiriki ipasavyo kuhakikisha kwamba nyenzo hizi mbili zinakidhi mahitaji ya nchi na matarajio ya serikali, niwahakikishie wizara kupitia Idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na COSTECH itazingatia maoni ya ushauri wenu katika kuboresha rasimu zote mbili," alisema.

Alitaja mafanikio yaliyopatikana wakati wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya Mwaka 1996 kuwa ni kuongezeka kwa taasisi za utafiti na maendeleo nchini kutoka 18 hadi 94.

Alitaja mafanikio mengine ni kuongezeka kwa vituo vya ubunifu na atamizi, vikifikia vituo 45 mwaka huu.

"Mafanikio mengine ni kuongezeka idadi ya watafiti kutoka taasisi za elimu ya juu na taasisi za utafiti na maendeleo za umma kutoka 3,593 hadi 10,966, kuibuliwa wabunifu na bunifu takribani 2,642 na kuimarisha nafasi ya Tanzania katika Global Innovation Index iliyopima uwezo wa nchi katika ubunifu wenye tija katika uchumi," alisema.

Pamoja na hayo, kiongozi huyo alisema kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) mwaka 1995 ambao hadi sasa umepokea zaidi ya Sh. bilioni 51.99, ni sehemu ya mafanikio ya sera hiyo.

Mkurugenzi wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, aliwaomba wadau kutoa maoni yao ili kuboresha sera hiyo itakayoleta mapinduzi kwenye masuala ya ubunifu.

Mkurugenzi wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu wa Wizara hiyo, Prof. Maulilio Kipanyula, alisema wamealika wadau 200 kwenye kikao hiko kutoka makundi mbalimbali katika sekta ya umma na binafsi wa Tanzania Bara na Zanzibar ili kupata wigo mpana wa wadau.



Mamalishe Roda Boy, akiandaa chakula kwa ajili ya wateja wake katika soko kuu la Majengo, jijini Dodoma jana. Kwa mujibu wa Roda, kazi hiyo inamwezesha kujikimu kimaisha ikiwa ni pamoja na kusomesha watoto wake. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wizara yageukia watoto walio mazingira hatarishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imesema imejipanga kuimarisha huduma za ustawi wa jamii nchini ikiwamo uratibu wa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Zainab Chaula, alibainisha hayo jana alipopokea gari lililotolewa na Shirika la PACT Tanzania kupitia mradi wa Achieve kwa ajili ya wizara kuimarisha huduma hizo.

Alisema wamejadiliana na shirika hilo katika kuboresha huduma kwa jamii na kuendelea kushirikiana kutekeleza miradi na programu mbalimbali hasa ustawi wa watoto na wazee ikiwamo afua za malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto na ustawi wa wazee nchini.

Katibu Mkuu alisema serikali inatekeleza majukumu mbalimbali kuhakikisha kero katika jamii zinatatuliwa, hivyo kwa kushirikiana na wadau itaharakisha kufikiwa kwa matokeo tarajiwa.

Dk. Chaula alitoa wito kwa wadau kuendelea kushirikiana na serikali kutoa huduma kwa wananchi na kuboresha miundombinu na vitendea kazi katika kufikia ustawi wa jamii.

"Sisi kama wizara tunaendelea kutoa wito kwa wadau wengine wajitokeze ili tuunganishe nguvu kwa pamoja kwani tunamsadia Rais Samia Suluhu Hassan kutoa huduma kwa wananchi," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la PACT Tanzania na mradi wa Achieve, Levina Kikoyo, alisema lengo la kutoa gari hilo ni kuhakikisha mifumo ya serikali inafanya kazi katika utekelezaji wa programu na huduma mbalimbali za ustawi ziwafikie walengwa.

"Tumefanya kazi na wizara hii kwa sababu katika huduma zetu tunafanya kazi ya kuwafikia watoto zaidi ya 600 nchini walio katika mazingira hatarishi hasa katika maambukizi ya VVU, lengo kuhakikisha watoto wanatambuliwa, wanapata huduma stahiki na dawa za kupunguza makali ya VVU," alisema.





# Wananchi wataka utafiti wa madhara kemikali migodini

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WANANCHI wilayani Chunya wameiomba Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) kufanya utafiti kwenye maeneo zinakofanyika shughuli za uchimbaji wa madini ili kutambua athari zitokanazo na matumizi ya kemikali.

Mkazi wa Itumbi wilayani hapo, Elika Solomon, alisema jana kuwa magonjwa katika maeneo wanayojihusisha na shughuli za uchimbaji madini ni mengi na chanzo chake huenda ni matumizi ya maji yenye kemikali kutoka migodini. "Huku porini Itumbi hakuna huduma ya maji, hivyo tunayatafuta kwenye mifereji au mito na ukiyatamaza hata kwa macho ni machafu lakini kwa sababu hatuna huduma hiyo, tunalazimika kuyatumia.

"Kitaalamu hatuwezi kujua ni athari gani tunaweza kuzipata, hivyo tunaomba Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu kutusaidia kufanya utafiti ili tuepukane na adha hiyo. Serikali pia itusaidie kujenga miundombinu ya mabomba ili tupate huduma ya maji katika eneo letu," alisema Solomon.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Dk. Daison Andrew, alisema shughuli za uchimbaji wa madini zina athari kubwa kwa jamii, hivyo kuna kila sababu kufanyika utafiti kwa kuzingatia sera ili jamii ipatiwe elimu ya kutambua madhara ya matumizi ya vitu vyenye kemikali hususani maji wanayotumia kuchenjua dhahabu.

"Jamii ikipatiwa elimu na kukubali kubadili mifumo ya uendeshaji wa maisha, itasaidia maeneo haya kubadili matumizi na kuokoa maisha ya wananchi wa Chunya.

"Kuna kitu cha kufanya kwa siku za mbeleni kwa watu kubadili mifumo ya maisha kwa kuachana na shughuli ambazo kwa namna moja ama nyingine zinahatarisha usalama wao kwa kuwa katika hatari ya kuibua magonjwa ya kansa," alishauri.

Dk. Andrew alisema katika maeneo hayo pia kuna ugonjwa wa kifua kikuu na kwamba yote hayo yanastahili kufanyiwa utafiti ili kusaidia kuokoa maisha ya wananchi wa Chunya.

Mkurugenzi Mkuu wa NIMR, Prof. Yunus Mgaya, alisema kila jambo linastahili ushirikishwaji na hivyo watashirikiana ili kuona namna ya kuwafikia kufanya utafiti wa kina kuhusu tatizo hilo.



Ofisa Mwandamizi wa Usamamizi wa Anga wa Uwanja wa Ndege wa Songwe, Emmanuel Wanje (kushoto), akitoa elimu kuhusu mawasiliano ya ndege yanavyofanyika kwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Atupele Mwakibete (katikati), alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa jengo la abiria na njia ya kutua ndege usiku uwanjani hapo, mkoani Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wizara: Sensa itasaidia kutambua mahitaji halisi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WIZARA ya Maji imesema Sensa ya Watu na Makazi itaisaidia kutambua mahitaji halisi ya maji yatakayowezesha kutoa huduma za uhakika za upatikanaji wake mijini na vijijini kwa kuzingatia idadi ya watu.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alitoa kauli hiyo juzi baada ya kushiriki sensa hiyo, akihesabiwa nyumbani kwake Iwambi jijini Mbeya.

Alisema taarifa sahihi za idadi ya watu na makazi zitaisaidia serikali kujua idadi kamili ya watu ili kutoa huduma za maji kulingana na mahitaji ya wananchi.

"Tunashukuru serikali tumefikia zoezi hili ambalo tulilisubiri kwa hamu kubwa, matumaini yetu ni kwamba tutapata takwimu sahihi za wananchi ili tuweze kutoa huduma stahiki ikiwamo ya maji ambayo yanategemea shughuli nyingine za maendeleo," alisema.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa kamili kwa makarani ili kuisaidia nchi kupata takwimu sahihi kwa ajili ya kufanikisha shughuli za maendeleo.

Alisema takwimu halisi za watu na makazi zitaisaidia serikali kujua mahitaji ya wananchi na hivyo kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kutoa huduma kulingana na idadi yao na kuwezesha nchi kufikia uchumi wa kati na kuboresha kipato cha kila Mtanzania.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema sensa ya mwaka huu inafanyika kidigitali na kazi imekuwa rahisi kuhesabu watu kulinganisha na miaka iliyopita.

Alisema miaka ya nyuma taarifa zilikuwa zinakusanywa kwenye karatasi na kulikuwa na ugumu kuzikusanya taarifa zote na kuzichakata.

# RC awataka walimu kuzingatia miongozo ufundishaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewataka walimu katika mkoa huo kuwafundisha wanafunzi kwa kuzingatia miongozo wanayopewa ili wapate maarifa ambayo serikali inakusudia.

Alitoa agizo hilo jana alipokuwa anafungua mkutano wa tathmini ya elimu katika mkoa huo uliowakutanisha wadau mbalimbali wa elimu.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Wakurugenzi wa Halmashauri, maofisa elimu, wakuu wa shule, maofisa kutoka Ofisi ya Mdhibiti Ubora wa Shule Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na maofisa kutoka Chama cha Walimu (CWT).

Alisema serikali inatoa miongozo ya elimu kulingana na mahitaji na kwamba ni lazima walimu wazingatie miongozo hiyo ambayo ni maalumu kwa ajili ya kuwanoa wanafunzi.

"Leo tunawakabidhi miongozo mipya ambayo mnatakiwa kwenda kuitekeleza kwenye vituo vyenu, hakikisheni mnazingatia haya mambo ili kufikia malengo ya serikali ambayo yamewekwa," alisema Homera.

Kadhalika alifafanua kuwa serikali imeweka mazingira mazuri ya kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaenda na ni wajibu wa wadau wote wa sekta hiyo kuhakikisha elimu inafikia malengo yake.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuboresha mazingira ya elimu ikiwa ni pamoja na kuweka mazingira bora ya walimu kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuboresha makazi na malipo.

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Ernest Hinju, alisema lengo la mkoa huo ni kuhakikisha wana faulisha wanafunzi wa ngazi zote kwa asilimia 100 na kwa mwaka ujao wanakusudia kushika nafasi ya kwanza kwa matokeo ya kidato cha nne.

Alisema ili kufikia malengo hayo ni lazima kila mdau atekeleze majukumu yake ipasavyo ikiwa ni pamoja na walimu kufundisha wanafunzi vizuri.

Mwaka uliopita mkoa huo ulishindwa kufikia baadhi ya malengo na kusema wanakusudia kuyafikia mwaka huu kwa kushirikiana na wadau.

Mkutano huo pia ulilenga kutoa mafunzo ya uongozi kwa viongozi hao wa elimu, kufanya tathmini ya elimu katika mkoa huo na kutangaza matokeo ya mtihani wa kujipima wa kidato cha nne uliofanyika mwezi Julai.





# TAMWA yataka usawa usimamizi wa uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar kimesema wakati umefika kwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) kuweka mazingira ya usawa wa kijinsia katika utekelezaji wa shughuli za tume, ukiwamo usimamizi wa uchaguzi.

Akizungumza jana katika mkutano wa kujadili Sera ya Jinsia uliofanyika katika ofisi ya ZEC, Mkurugenzi wa chama hicho, Dk. Mzuri Issa, alisema ushiriki wa wanawake katika shughuli za tume hiyo utaleta mwanga zaidi na kuwafanya wanawake wengi kufikia malengo yao yakiwamo ya kuwa viongozi.

Alisema kwa miaka mingi katika kazi za tume hiyo kumeonekana wanaume wengi ndiyo wanaoshiriki shughuli za tume, ukiwamo usimamizi wa uchaguzi huku wanawake wakibaki nyuma licha ya kwamba wao ni wengi zaidi.

Alisema iwapo wanawake wengi watashiriki katika utendaji wa tume hiyo, kutaamsha ushiriki zaidi wa kundi hilo katika harakati za kuchagua na kuchaguliwa na hatimaye kuwa na idadi kubwa ya wanawake kutimiza ndoto zao za kuwa viongozi katika kuufikia usawa wa kijinsia.

"Hata kama ikitokea idadi kubwa ya wanawake hawakuomba nafasi kwenye tume, mnao wajibu wa kuweka kanuni ambazo zitalazimisha asasi za kiraia kupeleka idadi kubwa ya wanawake katika shughuli za tume zikiwamo za usimamizi wa uchaguzi unaofanyika kila baada ya miaka mitano," alisema.

Mkuu wa Miradi TAMWA, Ali Mohamed, alisema wakati mabadiliko hayo ya kuleta usawa wa kijinsia yanaendelea kufanyika, kuna haja kuwekwa mazingira wezeshi katika sheria ya vyama vya siasa ili kuwe na masharti ya kuwapo idadi sawa ya wagombea katika nafasi za uongozi.

Alisema kuwapo kwa sheria hiyo kutachochea kuwa na mazingira rafiki kwa wanawake wengi na kuondoa ukandamizwaji ambao kwa miaka mingi wanawake wamelalamika.

Mkurugenzi wa Uchaguzi ZEC, Khamis Kona Khamis, alisema mkutano huo wa majadiliano umekuja wakati mwafaka kwa kuwa sasa tume iko katika mchakato wa kulifanyika kazi suala hilo.

Alisema licha ya dosari kadhaa zilizopo, kwa kiasi kikubwa tume hiyo inaendelea kufanyia kazi masuala ya kijinsia na ndiyo maana baadhi ya wilaya, ikiwamo Kaskazini Unguja, maofisa wote wa tume hiyo ni wanawake.

Alisema TAMWA kwa kushirikiana na asasi zingine za kiraia wana wajibu wa kupeleka mapendekezo yao pale wanapoona kuna shida za mifumo na kwa kufanya hivyo, watasaidia utendaji kazi wa tume hiyo na kusukuma maendeleo ya taifa.



Mkurugenzi wa Uchaguzi Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, Khamis Kona Khamis (kulia), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, baada ya kumaliza kikao cha majadiliano kuhusu sera ya usawa wa kijinsia, Maisara Mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Misumeno ya moto yanaswa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MISUMENO ya moto minane inashikiliwa na Idara ya Misitu Zanzibar baada ya kukamatwa ikitumika kukata miti kinyume cha Sheria ya Misitu na Hifadhi ya Maliasili na Mazingira.

Ofisa Mwandamizi wa Idara ya Misitu, Said Bilali, alisema jana kuwa kwa mujibu wa sheria hiyo, ni marufuku watu binafsi kumiliki misumeno ya moto ambayo imepigwa marufuku baada ya matumizi yake kuchangia uharibifu wa mazingira.

Alisema utafiti uliofanywa unaonyesha wapo baadhi ya watu wakimiliki misumeno ya moto kinyume cha sheria na hivyo kusababisha uharibifu wa kukata miti ikiwamo minazi.

Alisema wapo baadhi ya wafanyabiashara na maduka ya watu binafsi wanauza misumeno ya moto, kitendo ambacho kinakwenda kinyume cha sheria tajwa.

"Tumekamata misumeno minane inayomilikiwa na watu mbalimbali ambayo walikuwa wakiimiliki kinyume cha sheria na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema.

Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Mazingira, Sheha Mjaja, alisema serikali imepiga marufuku umiliki wa misumeno ya moto baada ya kubainika kusababisha athari za uharibifu wa mazingira.

Alisema kwa mujibu wa sheria, ni Idara ya Misitu na Maliasili pamoja na Baraza la Mazingira wenye mamlaka ya kuingiza misumeno ya moto pamoja na baadhi ya taasisi za ulinzi kwa ajili ya shughuli za dharura.

"Watu wanaomiliki misumeno ya moto pamoja na wafanyabiashara wanaoingiza nchini, wajue kwamba wanakwenda kinyume cha sheria ambayo imepiga marufuku uingizaji wa misumeno ya moto pamoja na matumizi ya kawaida isipokuwa kwa dharura," alionya.

**"Tumekamata misumeno minane inayomilikiwa na watu mbalimbali ambayo walikuwa wakiimiliki kinyume cha sheria na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao," alisema.**

# Serikali yaona fursa za kukuza uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Suleiman Masoud Makame, amesema ushirikiano kati ya serikali na ofisi ya sekretarieti ya eneo la Soko Huria la Bara la Afrika (AFCFTA) utaisaidia serikali kufikia azma yake ya kukuza uwekezaji na uwezeshaji kupitia sekta ya uchumi wa buluu.

Aliyasema hayo jana Maisara mjini Zanzibar wakati akifungua mkutano wa wataalamu wa ofisi ya sekretariati ya eneo la soko hilo.

Waziri Masoud alisema Zanzibar ina fursa nzuri za uwekezaji wa kiuchumi hasa katika eneo la bahari ambapo zikitumiwa ipasavyo zitarahisisha lengo la serikali kufikia uchumi endelevu.

Alisema madhumuni ya mkutano huo ni kukaa pamoja na wataalamu wa sekretarieti ya eneo la soko hilo waliofika Zanzibar kufuatia wito wa Rais wa Zanzibar wa kuangalia jinsi gani sekretarieti kuisaidia Zanzibar katika kuvutia wawekezaji na kuandaa miradi ya vipaumbele vya uchumi wa buluu.

Masoud alisema Zanzibar ina fursa kubwa ya kunufaika na uchumi wa bahari katika sekta za utalii, uvuvi, mazao ya baharini, usafiri na usafirishaji baharini pamoja na miundombinu, nishati mbadala, mafuta na gesi na hata usimamizi wa matumizi endelevu ya bahari.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema mkutano huo utaisaidia wizara kufanikisha kupanga mikakati ya kipaumbele kufuatia mpango wa serikali wa kutanua maeneo ya kiuchumi kwa manufaa ya taifa.

Komla Bissi, Mkuu wa Ushauri kutoka sekretarieti hiyo, alisema ushirikiano wa pamoja na serikali utaleta fursa katika kuchochea maendeleo ya haraka nchini.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**LINUS PANCRAS KAMUGISHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha form four chenye index number **NP0764/0016/2013,** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia **IZIGO SECONDARY SCHOOL mwaka 2013.** Kwa yeyote aliyekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

**POLISI TAARIFA :DAR/CHU/RB/335485/2022.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 91 OF 2022**
**In the Matter of the Estate of the Late:**
**ELIEZER HEZRON MALEKELA**

**BY 1. JOSEPH MWENYASI SANGALI**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 5 day of SEPTEMBER.........2022

**Dated at MOROGO this 22 day of AUGUST.........2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FAIR DEAL AUTO PVT LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Bajaj **BOXER** namba za usajili **MC 415 AUJ. Chassis no. MD2A21BZ2FWC73072,** Engine **No. PFZWFC76796.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/336548/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJ

**GLADNESS ISAYA LYOVA** Anatangaza kupotea kwa kadi za **BAJAJ** zenye namba za usajili **MC 938 BPS** yenye Engine Namba: **ZZWGB20325**

Na Bajaj yenye Namba za usajili **MC 216 BRY** yenye Engine Namba: **AZZWGE00416.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi taarifa ya Polisi RB Namba **IRI/IRI/RB/127930/2022 (MC 938 BPS)** **Na IRI/IRI/RB/12932/2022 (MC 216 BRY)**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NETO BEATUS MSEMBELE WA RUHUWIKO - SONGEA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye Namba za usajili **MC 600 AZU** aina ya **SNLG** kwa Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.


**TAARIFA YA POLISI: SO/RB/4792/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUNUS HASSAN MFALLA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya scania yenye usajili namba **T278 DGX , CHASSIS NAMBA XLER6X20004417014, ENGINE NAMBA 85913.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarfifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/330126/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMANUELA R. HHAYUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index Namba **S2264/0016** kilichotolewa mwaka 2010 na Baraza la Mitihani Tanzania **(NECTA)** kupitia shule ya sekondari Hanan'g.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu.

**Taarifa ya polisi: MAN/BAB/RB/109309/2022**

## KUPOTEA KWA YVETI



**IRENE HILDA MADEJE** anatangaza kupotea kwa vyeti vya taaluma; cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0214-0050** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MSALATO SECONDARY SCHOOL** mwaka 1991 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **SS0350-0526** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHYCOM HIGH SCHOOL mwaka 1994.** Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: KW/RB/3165/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GRACE LEVI MGENI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 398 AMF.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

**POLISI TAARIFA: IRI/IRI/RB/334319/2022**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676*

*OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni IndustRial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 0782253676*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wananchi wapewa miezi mitatu kuhama

**Na Said Hamdani,** LINDI

UONGOZI wa Halmashauri ya Mtama, Mkoa wa Lindi umewataka wananchi 248, wanaodaiwa kuvamia shamba linalomilikiwa na Kampuni ya Maumbika Plantation Farm, Kata ya Kiwalala kuondoka wenyewe ndani ya muda wa miezi mitatu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, George Mbilinyi, ametoa amri hiyo kupitia barua yake aliyomwandikia Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Frank Lukanga, ambaye naye aliisoma kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya ofisi ya Kata ya Kiwalala, Agosti 19 mwaka huu.

Barua hiyo yenye Na.LDW/V.20/1/211 ya Agosti 15/2022, na kutiwa saini na George Mbilinyi kwenda kwa ofisa mtendaji huyo inamjulisha kufutwa shamba Na. 37 lililoko eneo la Maumbika wilayani Mtama lililokuwa linamilikiwa kwa hati namba 5438.

"Ninapenda kuwajulisha rasmi kuwa, shamba tajwa hapo juu miliki yake imefutwa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi," ilisomeka sehemu ya barua hiyo.

Ilibainishwa zaidi katika barua hiyo kuwa shamba hilo limekabidhiwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mtama kwa barua Na.LD8671/26 ya Aprili 16, 2021 na kwamba halmashauri inaandaa mapendekezo ya matumizi mapya ya ardhi baada ya kufanya mpango.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Kiwalala, Lukanga, akiwasomea wananchi waliojitokeza kuitikia wito huo, alibainisha kumetolewa notisi ya siku 90, kwa wanaofanya makazi ndani ya shamba hilo kuondoka na atakayekaidi ataondolewa kwa nguvu kwa gharama zake mwenyewe.

Alisema, barua hiyo inataka mtu au watu wanaohitaji kuendelea kuwapo ndani ya shamba hilo, kuonana na mkurugenzi huyo ili kupewa maelekezo.

Wakizungumza katika mkutano huo uliomalizika bila kupata mwafaka, wananchi hao walitaka kufahamu mamlaka aliyopewa mkurugenzi huyo ya kuwaondoa bila kukutana nao.

Wananchi hao walisema, wanaishi kwenye shamba hilo baada ya kuruhusiwa na serikali ya awamu ya tatu kutokana na mmiliki wake waliyemtaja kwa jina la M/S Mathuradas Khalidas & Company Ltd, (Dewa) kudaiwa kulitelekeza miaka mingi iliyopita.

"Jeuri ya kutuondoa huyu mkurugenzi anaipata wapi? Tunaishi hapa kwa kuruhusiwa na serikali ya awamu ya tatu kupitia aliyekuwa Waziri Mkuu, Fedrick Sumaye," walidai Juma Abdullahamani na Mwanaidi Yusufu.

Hata hivyo, baada ya kuibuka maswali mengi yasiyo na majibu, Ofisa Mtendaji wa Kijiji, Frank Lukanga, aliondoka kwenye viwanja vya ofisi ya kata na kuingia ndani ya gari dogo na kuondoka eneo hilo, akiwaacha wananchi wakiendelea kufoka wakimtaka mkurugenzi kwenda kukutana nao.

# ACB yapania kufikisha mawakala 2,000

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Biashara ya Akiba (ACB) imeendelea kupanua wigo kwa kuanzisha huduma za wakala na inatarajia kufikia mwishoni mwa mwaka huu wawe wamefikia mawakala 2,000.

Magreth Mwasumbi, Meneja Mwandamizi wa Huduma za Kidijitali kwa ACB, Akiba, alisema jana kuwa huduma hizo zitasambaa nchi nzima ili kuwafikia wateja kwa karibu zaidi.

Huduma za wakala za ACB zilizinduliwa rasmi Agosti, mwaka jana na hadi sasa wamefikia 1,500 na wanatoa huduma za kibenki sehemu mbalimbali za Tanzania.

Mwasumbi alisema huduma za wakala zimeleta unafuu mkubwa katika upatikanaji wa huduma za kibenki kwa wateja wa ACB kwa kuwa watu wengi zaidi wamefikiwa na wanapata huduma kwa haraka na urahisi.

Alitoa rai kwa Watanzania wengi kujiunga na ACB ili kunufaika na fursa mbalimbali ndani ya benki hiyo, hususani za kidijitali ambazo zinaleta wepesi, unafuu na uharaka wa upatikana huduma.

Pia alisema benki inaendelea kuboresha na kuanzisha huduma nyingine nyingi za kidijitali kwa ajili ya kuwawezesha wateja kufanya miamala kwa haraka zaidi ndani na nje ya nchi.

Mmoja wa wateja wa benki hiyo, Krantz Mwantepele, ambaye ni mteja wa tawi la Ubungo, alisema jana kuwa huduma ya Akiba Wakala imemsaidia kupata mahitaji ya kibenki hata baada ya saa za kazi za benki.

"Hii inanifanya niweze kufanya miamala kwa urahisi na gharama nafuu. Hakuna ulazima wa kwenda tawini tena hakika Akiba Wakala ni zaidi ya huduma kwa kuangalia faida lukuki zilizosheheni katika huduma," alisema.



Vijana wakisomba zege kwa ajili ya kuweka jamvi sehemu ya Kanisa la Wasabato Mbezi Luis, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania wanolewa utafiti, uhifadhi bahari Afrika Kusini

**Na Jenifer Gilla**

SHIRIKA la Aqua-Farm (AFO), kwa kushirikiana na Shirika la Nature Environment Wildlife and Film Making (NEWF), limefadhili mafunzo ya kuzamia baharini kwa Watanzania wanane kutoka taaluma za sayansi bahari, waandishi wa habari, wapigapicha na video nchini Afrika Kusini ili kuwajengea uwezo katika nyanja za utafiti na uhifadhi wa bahari.

Wanataaluma hao pia wamepatiwa mafunzo ya viumbe bahari ili wawe na uwezo wa kuwatofautisha na kujua tabia zao ili kurahisisha utendaji kazi wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa AFO, Jerry Mang'ena, alisema kuwa wameratibu mafunzo hayo ili kuwaongezea ujuzi wataalamu hao utakaowasaidia kuwaondolea vikwazo walivyokuwa wakikutana navyo kabla.

"Tumegundua kuwa kuna wanataaluma za viumbe wanakosa ujuzi wa kuzamia baharini na kutofautisha viumbe hao, hali inayorudisha nyuma utendaji kazi wao na kusababisha kukosa maandiko ya viumbe bahari yanayojitosheleza, kwa hiyo tumeona tuwape ujuzi huu ili kuziba hilo pengo," alisema Jerry.

Pia alisema hii ni mara ya pili wanashirikiana na NEWF, kutoa mafunzo hayo ambayo mpaka sasa jumla Watanzania 11, wameshapatiwa lengo likiwa kufikia wataalamu wabobezi wa kuzamia (Dive Masters) 100, na wazamiaji wa kawaida 100, mpaka kufikia mwaka 2030.

"Mpaka sasa tumefikia wanataaluma ya viumbe bahari na waandishi wa habari za mazingira, lengo ni kufikia taaluma zote zinazohusisha viumbe bahari ili kuwaongezea ujuzi huo, tunategemea kupeleka wataalamu wengine tena mwakani Mungu akitujaalia," alisema.

Naye Mkurugenzi wa NEWF, makao makuu nchini Afrika Kusini, Noel Kok, alisema wameshiriki kufadhili mafunzo hayo ili kuongeza idadi ya watu weusi kwenye taaluma ya viumbe bahari na kutengeneza mazingira ya ujuzi wa uzamiaji kuwa wa kila mtu na sio wazungu pekee ili kulinda na kutetea mazingira ya bahari yao.

"Waafrika wawe na uwezo wa kuvielezea vitu vinavyowahusu, haiwezekani mwandishi wa habari atoke Marekani aje kuandika habari za viumbe bahari wa Tanzania wakati nchi hiyo inayo waandishi wa habari. Tunataka tuondoe vikwazo vinavyosababisha kazi za wa Afrika kufanywa na wataaluma wa Ulaya," alisema.

Alisema, mpaka sasa mradi huo umeshawafikia Waafrika 120, kutoka taaluma mbalimbali na lengo ni kuwafikia wengi zaidi huku wanawake wakiwapa kipaumbele.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, mwanasanaa za vibonzo, Aika Kirei, alisema kupitia mafunzo hayo amejifunza aina na tabia za viumbe bahari na kuhamasika kuandika habari na kutengeneza vibonzo vitakavyolenga utunzaji wa viumbe wa bahari.

"Mafunzo haya yamenipa muhali ya kuandika habari za utunzaji viumbe bahari kwa sababu sasa hivi sihitaji mtu aniambie, naweza kwenda mwenyewe chini ya bahari na kuangalia usalama wao, kwa kweli nawashukuru sana AFO na NEWF," alisema Aika.

Wakati, mtaalam wa viumbe bahari, Arnold Shoko, alisema kuwa mafunzo ya kuzamia baharini yamemrahisishia utendaji wake wa kazi kwa sababu hapo mwanzo kazi ilikuwa ikichelewa kutokana na kupoteza muda mwingi kutafuta watu wa kwenda kuzamia.

Huku Mtaalam wa bioteknolojia, Clement Mlay, ambaye amekua akifanya utafiti wa namna viumbe bahari vinanvyo ingiliana kwa kutumia vinasaba amesema:

"Mwanzo ilikuwa unapoteza muda kutafuta watu wa kwenda kuzamia kukufanyia kazi yako kwa sababu nilikuwa sina ujuzi, pia nilikuwa natumia pesa nyingi kuwalipa watu hao na wakati mwingine wanakuletea kitu tofauti na ulichowatuma, lakini sasa hivi kila kitu kitakuwa sawa," alisema.

# SIMBA QUEENS NA HESABU KWA SHE CORPORATES FAINALI CECAFA

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuichapa She Corporates ya Uganda mabao 2-0, walipokutana kwenye hatua makundi, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema hawatawachukulia poa wapinzani wao hao katika mchezo wao wa fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa CECAFA ya Wanawake.

Simba Queens imetinga fainali kwa kishindo baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya AS Kigali ya Rwanda katika mchezo wa nusu fainali ya pili iliyopigwa juzi Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Katika nusu fainali ya kwanza juzi, She Corporates nayo iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya CBE FC ya Ethiopia, hivyo sasa itakutana na Simba Queens kwenye mechi ya fainali itakayopigwa kesho katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nkoma alisema wamejiandaa vizuri kukabiliana na She Corporates na wanatambua ubora wa wapinzani wao, hivyo wanapaswa kuwa makini na kuwaheshimu.

Kuhusu nafasi ya makipa, alisema ana waamini na ana matarajio makubwa kutoka kwa nyota wake hao kufanya vizuri katika nafasi hiyo.

"Tumejipanga vizuri katika mchezo wetu wa nusu fainali dhidi ya As Kigali, nawapongeza wachezaji wangu kwa kupambana kupata matokeo mazuri katika mchezo huo kwa sababu wapinzani wetu hao si wabaya," alisema Nkoma.

Alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu katika mchezo wa hatua ya makundi alikutana nao na walicheza kwa ushindani mkubwa.

"Tumejiandaa vizuri, She Corporates ni timu nzuri na mechi ya kwanza tuliwafunga kwa mbinu, kwa hali hiyo tunahitaji kujipanga zaidi na kucheza kwa nidhamu kubwa ili kufikia malengo yetu ya kutwaa ubingwa wa CECAFA," alisema Nkoma.

Bingwa wa michuano hiyo mbali ya kuuwakilisha Ukanda wa CECAFA kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika baadaye mwaka huu nchini Morocco, pia ataondoka na Kombe na Dola za Marekani 30,000 huku mshindi wa pili akibeba dola 20,000 na watatu akiambulia dola 10,000.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Diana William, akipongezwa na mchezaji mwenzake, Kiungo Vivian Aquino, baada ya kuifungia timu yake bao la nne wakati ikishinda 5-1 dhidi ya AS Kigali ya Rwanda kwenye mechi ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake Ukanda wa CECAFA, iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Karia awataka wanachama CECAFA kufuata ratiba CAF

**Na Saada Akida**

RAIS wa Baraza la Vyama na Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), pia Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania, Wallace Karia, amesema wanapambana kuhimiza vyama kuanza ligi mapema ili kuendana na ratiba ya mashindano ambayo yanasimamiwa na baraza hilo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Karia alisema wanahitaji kukaa na kuangalia mashindano ya CECAFA ambayo wanahitaji kuyafanya ikiwamo michuano ya Kombe la Kagame kwa ngazi ya klabu na timu za taifa.

"CECAFA tutaheshimu ratiba ya CAF kwa kuhakikisha hilo tumeomba vyama vya ukanda huu kuzingatia ligi zao zinaanza mapema, hadi sasa Sudan bado ligi zinaendelea wakati kwa Tanzania tumeanza msimu mpya.

"Tanzania tunahitaji kumaliza ligi Mei mwakani, kwa ajili ya kujipanga ratiba yetu ili kuweza kuwapa nafasi wachezaji kupumzika, pia kufanya mashindano yetu ikiwamo Kagame Cup kwa ngazi ya klabu," alisema Karia. Alisema CECAFA nia yao ni kucheza mashindano yote ikiwamo ya wanaume na wanawake kwa miaka mbalimbali pamoja na vijana.

"Kuelekea michuano ya Kombe la Dunia na CHAN, imekuwa ngumu na hatua hii imebadilisha ratiba yetu na kuhakikisha tunaandaa mashindano yetu kulingana na kufuata Kalenda ya CAF," alisema Karia.

Alisema kwa sasa wanaangalia na Kalenda ya CAF kutokana na utaratibu wa mashindano ya Afrika Super Ligi jinsi gani wanashiriki ili kuangalia uwezekano wa kuandaa mashindano yao.

Aidha, Karia alisema Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, amekuwa chachu kubwa ya mashindano ya CECAFA kwa Wanawake yanayoendelea Dar es Salaam kwa sasa, kutokana na kudhamini michuano hiyo kwa kuchangia katika zawadi.

"Haya mashindano kufanyika ni mara ya pili, mwaka jana yalifanyika Kenya na sasa Tanzania ni wenyeji, ambayo tutapata mwakilishi kwa Ukanda wa CECAFA ili kupata mwakilishi katika Ligi ya Mabingwa itakayofanyia nchini Morocco.

"Tumshukuru Mama Samia kuunga mkono michezo hasa mpira wa miguu kutoa zawadi kwa bingwa wa michuano hii ambaye atachukuwa Dola za Marekani 30,000, wa pili dola 20,000 na mshindi wa tatu akiondoka na dola 10,000," alisema Karia.

# Ahmadiyya Cup yatimua vumbi Dar

**Na Isiyaka Nyamihasi,** TUDARCo

KUELEKEA Mkutano Mkuu wa mwaka wa Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya, imeandaa mashindano ya mpira wa miguu yaliyoanza kutimua vumbi Agosti 21, mwaka huu katika viwanja vya Sekondari ya Ahmadiyya iliyopo Kata ya Msongora, Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam.

Katika mashindano hayo yanayoshirikisha timu 16 zote kutoka Dar es Salaam, yanatarajiwa kumalizika Septemba 25, mwaka huu huku zawadi mbalimbali zikiwamo kombe, ng'ombe, mbuzi na jezi zikitolewa kwa washindi.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mwenyekiti wa Mashindano hayo, Hamidii Kaigwa, alisema lengo la mashindano hayo ni kukuza vipaji vya wachezaji, kujenga afya ya mwili na kuutangaza mkutano huo utakaofanyika kuanzia Septemba 30 hadi Oktoba 2, mwaka huu, ambao pamoja na mambo mengine, lengo likiwa ni kuhamasisha amani na upendo katika jamii.

"Tutatoa zawadi kwa mshindi wa kwanza mpaka wa tatu, mshindi wa kwanza atapata kombe, ng'ombe mmoja, seti ya jezi na mpira, wa pili atazawadiwa mbuzi mmoja, seti ya jezi na mpira na wa tatu atapewa seti ya jezi na mpira," alisema Kaigwa.

Kwa upande wa mchezaji wa timu ya Safina Athletic FC inayoshiriki mashindano hayo, Ismail Abdul-nasibu, alisema ni furaha kwake kupata nafasi ya kushiriki michuano hiyo kwani mbali ya kuinua na kukuza vipaji vya wachezaji ni fursa kwake kujitangaza.

"Ninafuraha kubwa kushiriki mashindano haya, kwanza hakukuwa na tozo ya kujiunga kushiriki, lakini tutapata changamoto tukikutana wachezaji mbalimbali na tutakuza vipaji vyetu na kujenga afya za miili yetu,"alisema.

Miongoni mwa timu zinazoshiriki mashindano hayo ni pamoja na Msongola Veterans FC, St. Emanuel FC, Azam B FC na Ahmadiyya Sekondari FC.

# Taifa Queens yapigwa kufuzu Kombe la Dunia

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa Netiboli Tanzania (Taifa Queens ), imeanza vibaya mashindano ya Afrika kuwania kufuzu Kombe la Dunia, yanayoendelea Pritoria, Afrika Kusini baada ya kupoteza michezo yake mitatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, moja kwa moja kutoka Afrika Kusini, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Hafidhi Tindwa, alisema sababu ya kupoteza michezo hiyo ni kutokana na kuzidiwa ufundi.

"Tumepoteza michezo miwili mpaka sasa, nimebaini mapungufu machache ambayo nitayafanyia kazi ili tutimize malengo yetu," alisema Tindwa.

Kocha huyo alisema mchezo wa kwanza walipoteza kwa mabao 54-40 dhidi ya wenyeji, Afrika Kusini na kisha kuchapwa 43-33 dhidi ya Zimbabwe kabla ya kunyukwa 54-45 na Botswana.

## ZISIKUPITE

### ISAK ATENGEWA FUNGU



KLABU ya Newcastle United imeweka rekodi ya klabu kutenga kitita cha pauni milioni 60 kumnunua mshambuliaji wa Real Sociedad mwenye umri wa miaka 22, Alexander Isak. ***(Mail)***

### CHELSEA KUMNUNUA MAGUIRE

CHELSEA huenda ikamnunua mlinzi wa Manchester United na England, Harry Maguire mwenye umri wa miaka 29, ikiwa hawataweza kumsajili mlinzi wa kati wa Ufaransa, Wesley Fofana mwenye umri wa miaka 21, kutoka Leicester. ***(Evening Standard)***

### ANTONY BEI JUU




KLABU ya Ajax inataka pauni milioni 84 ili kumwachia winga wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 22, ambaye amedhamiria kuhamia Manchester United. ***(Telegraph)***

### JONG ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wametoa ofa kwa Barcelona kumnunua kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25. ***(Futbol Total, via Forbes)***

### PAQUETA HATAKIWI ARSENAL




ARSENAL haitarajiwi kumnunua Lucas Paqueta licha ya ripoti kuwa wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Express)***

### NILES AWANIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imepewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Arsenal na England, Ainsley Maitland-Niles mwenye umri wa miaka 24 katika wiki za mwisho za dirisha la uhamisho. ***(Mail)***

### DUBRAVKA AWINDWA UNITED



KLABU ya Manchester United imefanya mazungumzo na Newcastle United kuhusu kumsajili mlinda mlango wa Slovakia, Martin Dubravka mwenye umri wa miaka 33. ***(Mail)***

### SILVA HAONDOKI

MTENDAJI Mkuu wa Manchester City, Ferran Soriano amefutilia mbali uwezekano wa kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 28, kuihama klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. ***(SER Catalunya, via 90min)***

### VILLA YASHUSHA DAU



KLABU ya Aston Villa imeshusha dau kwa mlinzi Frederic Guilbert huku wakitafuta kumuuza Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 27. ***(L'Equipe, via BirminghamLive)***

### AURIER ATAKIWA FOREST

KLABU ya Nottingham Forest ina nia ya kumsajili mlinzi wa kulia wa Ivory Coast, Serge Aurier mwenye umri wa miaka 29, ambaye anapatikana kwa uhamisho wa bila malipo baada ya kuondoka Villarreal. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AFUNGUKA SILVA KWENDA BARCA

**MANCHESTER,** England

**Tunamtegemea na sitaki aondoke, lakini sitaki mchezaji akose furaha, ikiwa ofa nzuri...**

PEP Guardiola hajapuuza uwezekano wa Bernardo Silva kujiunga na Barcelona - klabu ambayo "anaipenda sana" - lakini amekiri kuwa dili hilo litakuwa gumu katika kipindi hiki cha dirisha la uhamisho wa majira ya joto linaloelekea ukingoni.

**Silva anasalia kuwa mtu muhimu kwa Manchester City ya Guardiola, akifanya vema na kufunga bao la kusawazisha Jumapili katika sare ya 3-3 dhidi ya Newcastle United, lakini pia anaendelea kuhusishwa na Barca.**

'The Blaugrana' hao wamewekeza fedha nyingi kwenye dirisha hili, huku Robert Lewandowski, Raphinha na Jules Kounde wakiwa miongoni mwa wachezaji waliowasajili.

Hata hivyo, kocha wa Barca, Xavi anasemekana kuwa bado ana nia ya kuongeza wachezaji zaidi, huku Silva akionekana kuwa mchezaji muhimu wa kumnasa.

City walicheza na Barca pale Camp Nou Jumatano kwenye mechi ya hisani ambayo ilimalizika kwa sare ya mabao 3-3 - na makocha wote wawili Xavi na Guardiola walizungumza kuhusu Silva baada ya mechi.

"Nani hampendi Bernardo Silva? Kama De Bruyne au Haaland," alisema Xavi. "Lakini hakuna habari zaidi. "Ni mchezaji ninayempenda - ni wachache kama yeye, lakini inategemea na City."

Maneno hayo yalimpa Guardiola fursa ya kuwa na usemi wa uhakika juu ya mustakabali wa Silva, lakini alirudia maneno yake kwamba, angetaka tu kumbakisha mchezaji mwenye furaha hapo City.

"Tunamtegemea na sitaki aondoke," alisema Guardiola. "Yeye ni mchezaji bora katika kila kitu anachofanya.

"Lakini kama ninavyosema siku zote: Sitaki mchezaji akose furaha. Ikiwa ofa nzuri itakuja na mwenyewe anataka kuondoka haina shida.

"Ingawa akiondoka sasa itakuwa ni shida maana soko linakaribia kufungwa. Nafahamu kwamba, Bernardo anaipenda sana Barcelona."

Dirisha litafungwa Alhamisi ijayo, huku biashara ya City ikionekana kukamilika baada ya kuwaongeza Erling Haaland, Stefan Ortega, Kalvin Phillips na Sergio Gomez kwenye kikosi cha Guardiola, pamoja na Julian Alvarez, ambaye alisajiliwa Januari.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,025,1

MECHI KALI
LAZIO
VERSUS
INTER
1 | 3.79
X | 3.69
2 | 1.83

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
BREAKING
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# PEPE ARUDI UFARANSA KWA MKOPO




**PARIS,** Ufaransa

ARSENAL, wamefikia makubaliano na Nice kumtoa kwa mkopo winga wa Ivory Coast, Nicolas Pepe, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 72 mwaka 2019, Pepe amefunga mabao 27, pekee katika mechi 112, alizoichezea Arsenal na amekua hana nafasi chini ya Mikel Arteta, akianza mechi tano tu za Ligi Kuu msimu uliopita na hajacheza kabisa msimu huu.

'Washikabunduki' hao wamekuwa na nia ya kusajili winga mpya wa kulia msimu huu - Pedro Neto wa Wolves yuko kwenye rada zao - lakini walihitaji kumuuza Pepe ili kutoa nafasi kwa mchezaji yeyote mpya.

Vyanzo vimethibitisha kwamba 90min, Nice ya Ligi Kuu Ufaransa imefikia makubaliano ya kumsajili Pepe kwa mkopo wa mwaka moja, katika hatua ambayo haitajumuisha chaguo la kumnunua. Pepe, anaifahamu vyema Ligue 1, baada ya kung'ara akiwa na Lille msimu wa 2018/19 kabla ya kuhamia Arsenal.

Raia huyo wa Ivory Coast, alipachika mabao 23, na kutoa pasi za mabao 12 katika michuano yote mwaka huo.

Kwa kuwa kuna nafasi kwenye kikosi, Arsenal wanatumaini kusajili fowadi mpya na wako tayari kuongeza kasi ya kutaka kumnunua Neto.




# Bailly atua Marseille

**MARSEILLE,** Ufaransa

KLABU ya Marseille imekamilisha usajili wa beki wa Manchester United, Eric Bailly kwa mkopo na chaguo la kumnunua.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, amekuwa na wakati mgumu tangu alipohamia Old Trafford kutoka Villarreal mwaka 2016, kutokana na majeraha na kiwango duni kilichomfanya kucheza mechi 113, tu katika kipindi cha miaka sita akiwa United.

Msimu wake wa kwanza ulikuwa mwaka pekee ambao alicheza mechi zaidi ya 13 za Ligi Kuu.

Bailly, alicheza dakika 487 mwaka jana na sasa amepewa nafasi ya kujiimarisha upya kule Marseille. Kikosi hicho cha Ufaransa kimemsajili Bailly kwa mkopo kwa msimu mzima ambao unajumuisha chaguo la kumnunua, huku ripoti zikisema hilo litakuwa jukumu ikiwa atacheza michezo ya kutosha na Marseille kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Bailly ataisaidia Marseille kuziba pengo lililoachwa wazi na William Saliba, ambaye amerejea Arsenal na pia ataungana na Nuno Taveres anayecheza kwa mkopo Arsenal.

118,259/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 27/08/22 | 17:00 | Blackpool vs Bristol City | 2.28 | 3.19 | 3.19 |
| 02. 27/08/22 | 17:00 | Cardiff vs Preston | 2.54 | 3.08 | 2.89 |
| 03. 27/08/22 | 17:00 | Hull City vs Coventry | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 04. 27/08/22 | 17:30 | GO Ahead Eagles vs Sparta Rotterdam | 2.33 | 3.53 | 2.84 |
| 05. 27/08/22 | 19:30 | Juventus vs Roma | 2.31 | 3.19 | 3.14 |
| 06. 27/08/22 | 19:30 | Cremonese vs Torino | 2.99 | 3.34 | 2.32 |
| 07. 27/08/22 | 21:45 | Spezia vs Sassuolo | 2.99 | 3.39 | 2.29 |
| 08. 27/08/22 | 22:00 | Lens vs Rennes | 2.44 | 3.36 | 2.76 |
| 09. 28/08/22 | 01:00 | Fluminense vs Palmeiras | 2.60 | 3.15 | 2.75 |
| 10. 28/08/22 | 14:00 | Nantes vs Toulouse | 2.40 | 3.27 | 2.88 |
| 11. 28/08/22 | 14:30 | KAA Gent vs Royal Antwerp | 2.34 | 3.43 | 2.89 |
| 12. 28/08/22 | 14:30 | Hannover vs Greuther Furth | 2.79 | 3.39 | 2.43 |
| 13. 28/08/22 | 15:15 | FC Lugano vs St. Gallen | 2.45 | 3.49 | 2.69 |
| 14. 28/08/22 | 16:00 | Aston Villa vs West Ham | 2.37 | 3.24 | 2.99 |
| 15. 28/08/22 | 16:00 | Wolverhampton vs Newcastle | 2.64 | 3.19 | 2.69 |
| 16. 28/08/22 | 16:00 | Nice vs Marseille | 2.48 | 3.33 | 2.73 |
| 17. 28/08/22 | 16:00 | Troyes vs Angers | 2.53 | 3.18 | 2.78 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 26 - AGOSTI 2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2004 | Sagan Tosu vs Avispa Fukuoka | 2.17 | 2.99 | 3.29 |
| 14:30 | 2323 | Beijing Guoan vs Shanghai Shenhua | 2.12 | 3.28 | 3.08 |
| 14:45 | 3555 | Hougang United vs Lion City Sailors | 5.60 | 5.20 | 1.41 |
| 15:00 | 1587 | Port FC vs Prachuap FC | 1.70 | 3.65 | 4.24 |
| 17:00 | 1370 | Misr Lel Makasa vs Smouha Club | 7.04 | 4.12 | 1.45 |
| 17:00 | 3656 | MSK Zilina vs Zemplin Michalovce | 1.73 | 3.72 | 3.92 |
| 17:30 | 3453 | Aluminium Arak vs Persepolis FC | 6.29 | 2.70 | 1.75 |
| 18:30 | 5812 | Tabor Sezana vs ASK Bravo | 2.35 | 3.09 | 2.84 |
| 18:45 | 1477 | Voluntari vs Universitatea Cluj | 2.19 | 3.05 | 3.40 |
| 18:45 | 2867 | CS Constantine vs USM Khenchela | 1.36 | 4.11 | 8.22 |
| 19:00 | 1700 | RC Arbaa vs MC Oran | 2.02 | 2.85 | 3.93 |
| 19:00 | 5418 | Karmiotissa vs Nea Salamis | 2.11 | 3.48 | 3.23 |
| 19:30 | 2968 | Neftchi Baku vs Zira | 2.11 | 3.10 | 3.29 |
| 19:30 | 3653 | Fortuna Dusseldorf vs Jahn Regensburg | 1.60 | 3.91 | 5.01 |
| 19:30 | 3858 | El Gouna vs Coca Cola | 2.38 | 2.96 | 3.16 |
| 19:30 | 4344 | Monza vs Udinese | 2.80 | 3.25 | 2.41 |
| 19:30 | 5064 | El Ittihad Alexandria vs Arab Contractors | 3.72 | 2.87 | 2.18 |
| 20:00 | 1044 | Sonderjyske vs Naestved BK | 1.60 | 3.77 | 4.80 |
| 20:00 | 3061 | Sochi vs FK Khimki | 1.62 | 3.95 | 4.79 |
| 20:00 | 3317 | Horsens vs Aarhus | 2.96 | 3.16 | 2.38 |
| 20:00 | 4504 | Vilafranquense vs CD Feirense | 2.59 | 3.13 | 2.64 |
| 20:30 | 5449 | Nancy vs Dunkerque | 2.17 | 3.13 | 3.28 |
| 21:00 | 1769 | Gaziantep BB vs Antalyaspor | 2.72 | 3.37 | 2.44 |
| 21:00 | 2116 | Ujpest FC vs Paksi FC | 2.19 | 3.52 | 2.79 |
| 21:00 | 3386 | Albacete Balompie vs Huesca | 2.31 | 3.04 | 3.14 |
| 21:00 | 3823 | NEC Nijmegen vs Groningen | 2.19 | 3.40 | 3.05 |
| 21:00 | 4414 | Spartak Subotica vs Backa Topola | 2.66 | 3.15 | 2.45 |
| 21:00 | 4792 | Eyupspor vs Yeni Malatyaspor | 1.32 | 4.72 | 7.68 |
| 21:00 | 5087 | Girona vs Celta Vigo | 2.77 | 3.07 | 2.61 |
| 21:00 | 5460 | FC Eindhoven vs Jong AZ Alkmaar | 1.66 | 3.94 | 4.39 |
| 21:00 | 5476 | PEC Zwolle vs Jong PSV | 1.40 | 4.59 | 6.59 |
| 21:15 | 3337 | NK Celje vs ND Gorica | 1.57 | 3.73 | 5.11 |
| 21:15 | 5687 | FC Wil vs FC Thun | 2.55 | 3.53 | 2.35 |
| 21:30 | 1377 | Chrobry Glogow vs Wisla Krakow | 3.52 | 3.33 | 1.94 |
| 21:30 | 2504 | UTA Arad vs U Craiova SA | 2.80 | 3.10 | 2.49 |
| 21:30 | 3450 | SC Freiburg vs VfL Bochum | 1.46 | 4.48 | 5.77 |
| 21:30 | 4431 | Ionikos Nikea FC vs Levadiakos | 2.17 | 3.21 | 3.31 |
| 21:30 | 4808 | Stal Mielec vs Legia Warszawa | 3.49 | 3.45 | 1.91 |
| 21:45 | 2026 | The New Saints vs Gap Connahs Quay | 1.48 | 4.24 | 5.32 |
| 21:45 | 2414 | Lazio vs Inter | 3.79 | 3.69 | 1.83 |
| 21:45 | 3508 | Bala Town vs Newtown AFC | 2.01 | 3.53 | 3.14 |
| 21:45 | 4482 | Charleroi vs Brugge | 3.51 | 3.61 | 1.95 |
| 21:45 | 5594 | Derry City vs Cork City | 1.30 | 4.43 | 9.46 |
| 22:00 | 1297 | Ceramica Cleopatra vs Pyramids | 4.82 | 3.51 | 1.72 |
| 22:00 | 1979 | Luton Town vs Sheffield Utd | 2.99 | 3.14 | 2.34 |
| 22:00 | 2746 | Al Masry Club vs Zamalek | 3.61 | 3.01 | 2.15 |
| 22:00 | 4804 | AC Ajaccio vs Lille | 3.20 | 3.15 | 2.24 |
| 22:15 | 2627 | Pacos Ferreira vs GD Estoril | 2.41 | 3.11 | 2.96 |
| 23:00 | 5378 | Betis vs Osasuna | 1.89 | 3.49 | 3.94 |
| 23:00 | 5733 | FC Cartagena vs Zaragoza | 2.34 | 3.14 | 2.99 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KIM: STARS KAMILI KUIVAA UGANDA KUFUZU CHAN



**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', Kim Poulsen, amesema kikosi chake kipo kamili kuelekea mchezo wa kesho dhidi ya Uganda baada ya kumaliza programu alizokuwa ameandaa.

**Taifa Stars, itakuwa mwenyeji wa mchezo huo wa raundi ya pili kuwania kufuzu Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wanaocheza Ligi za Ndani (CHAN), utakaochezwa kesho kabla ya kurudi ugenini Septemba 3, mwaka huu katika Uwanja wa St. Marys, Uganda.**

Akizungumza na gazeti hili jana baada ya mazoezi ya asubuhi, Poulsen alisema, aliandaa programu kwa nyota wake ambayo kila siku walikuwa wanaifanya katika nafasi tofauti na anaamini amefanikiwa.

"Nilianza kwa walinzi, tukafuata kwa washambuliaji na leo tumeelewana na tupo tayari kwa ajili ya mchezo wa kwanza," alisema Kim.

Naye kipa wa timu hiyo, Aishi Manula, alisema wanamshukuru Mungu kwa kumaliza maandalizi salama na kwa upande wao, watapambana kuhakikisha wanaanza vizuri nyumbani.

Alisema, Uganda ni timu ambayo wanafahamiana na hata kocha amekiandaa kikosi chake kwa jinsi anavyowafahamu wapinzani wao.

"Utakuwa mchezo mgumu, lakini kwanza tunahitaji matokeo mazuri tukiwa nyumbani kabla ya kurudiana, itakuwa mechi ya ushindani kwa sababu nao wanakikosi kizuri," alisema.

Taifa Stars, imetinga hatua ya pili baada ya kuitoa timu ya Taifa ya Somalia katika michezo ya hatua ya kwanza kwa jumla ya mabao 3-1 kwenye mbio hizo za kuelekea CHAN zitakazofanyika Januari mwakani nchini Algeria.

## Minziro ataka 4 za kirafiki kabla kuwavaa Wasudan



**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold, Fred Ferix Miziro, amesema anahitaji kupata mechi tatu au nne za kirafiki kabla ya kukutana na Hilal Alsahil, ya Sudan katika mechi ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayopigwa kati ya Septemba 9-11, mwaka huu.

Katika michuano hiyo, ambayo Geita Gold itashiriki kwa mara ya kwanza, itaanzia ugenini na mshindi wa jumla atakwenda kukutana na Pyramids ya Misri kwenye raundi ya kwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Minziro alisema, kikosi chake hakijapata mechi nyingi za kirafiki kabla ya ligi kuanza, hivyo ataueleza uongozi uweze kumfanikishia matakwa yake hayo ya mechi za kirafiki.


"Nahitaji kufanya mazungumzo na uongozi wa klabu kuona kama tutaweza kufanikisha kupata mechi tatu au nne za kirafiki kabla ya kuanza kwa michuano ya kimataifa.

"Wachezaji wangu hawajakaa pamoja kwa muda mrefu kuweza kujuana, hivyo naamini tukicheza mechi hizo za kirafiki, kila kitu kitakuwa sawa na sisi ndio mara ya kwanza kushiriki michuano hii tunahitaji kuwa imara zaidi, " alisema Minziro.

# Michezo

Ijumaa Agosti 26, 2022

Nipashe

Guardiola afunguka Silva kwenda Barca UKURASA 21

POZA KOO...



Washambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (kushoto) na Aziz Ki wakipoza koo kwa maji wakati wa mazoezi. **PICHA: MAKTABA**

# Yanga yataja mechi 3 ngumu za ushindi

**Na Saada Akida**

## ●●● Nabi azipangia programu akataa mechi za kirafiki, asema...

UONGOZI wa Yanga umeweka wazi mikakati yao kuelekea michezo minne iliyopo mbele yao ikiwamo miwili ya Ligi Kuu Tanzania Bara na idadi kama hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo inatarajiwa kuchezwa Septemba 10, mwaka huu.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Mkurugenzi wa mashindano wa Klabu ya Yanga, Saad Kawemba, alisema kikosi chao kinaendelea na mazoezi kujiandaa na michezo minne ambayo alidai ni migumu na yenye ushindani mkubwa ndani ya siku 11.**

Alisema kati ya mechi hizo mbili za Ligi Kuu Tanzania Bara, watacheza dhidi ya Azam FC na Mtibwa Sugar Septemba 6 na 13, mwaka huu, mechi ambazo alidai ni ngumu kupata ushindi.

"Tunahitaji kupata matokeo mazuri katika michezo hiyo miwili, lakini tuna mechi mbili za kimataifa dhidi ya Zalan FC, ambazo tutacheza Septemba 10 na 17 mwaka huu, tutarudiana.

"Katika michezo yote, tunahitaji kushinda, ikiwamo michuano ya kimataifa kwa akili ya kufikia malengo yetu ya kucheza hatua ya makundi," alisema Kawemba.

Alisema wana matarajio makubwa ya kufanya vizuri katika michezo ijayo ikiwamo ya kimataifa kwa sababu malengo yao makubwa ni kuona timu hiyo inafanya vizuri na kucheza hatua ya makundi.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema hakupata maandalizi mazuri ya msimu mpya kabla ya ligi kuanza, hivyo anatumia kipindi hiki kukiandaa kikosi chake.

"Nataka kutumia hizi siku kufanya mazoezi ya nguvu ili ifidie zile siku tulizokosa 'preseason', hivyo hatutakuwa na mchezo wa kirafiki," alisema Nabi.

Alisema baada ya juzi kuanza mazoezi ya 'gym', jana kikosi chake kimeanza mazoezi ya uwanjani akiwa na lengo la kutengeneza muunganiko ambao anautaka.

"Tumecheza michezo miwili ya ligi licha ya kushinda mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania na 2-0 dhidi ya Coastal Union, bado sijaridhishwa na muunganiko wa timu yangu," alisema.

Naye kiungo mshambuliaji wa Yanga, Bernard Morrison, alisema kulingana na ratiba iliyopo mbele yao, wamelazimika kukatisha mapumziko yao na kuendelea na maandalizi ya michezo iliyopo mbele yao ukiwamo dhidi ya Azam FC.

Alisema mechi zilizopo mbele yao hasa mchezo dhidi ya Azam FC ni muhimu kupambana kupata matokeo mazuri ili kufikia malengo yao ya kukusanya pointi kila mechi.

"Tumekatisha mapumziko kwa ajili ya kurejea mazoezini kujiandaa na michezo iliyopo mbele yetu ikiwamo dhidi ya Azam FC, mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa kwa sababu ya kila timu kutafuta matokeo," alisema Morrison.

# Simba SC yapaa Sudan na nyota 19

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji 19 wa Simba, benchi la ufundi na baadhi ya viongozi kimeondoka leo alfajiri nchini kwenda nchini Sudan kupitia Ethiopia kwa ajili ya kushiriki michuano maalum iliyoandaliwa na Klabu ya Al Hilal ya nchini humo, imeelezwa.

Awali, Simba ilitarajia kuondoka jana, lakini ikaahirisha na kutangaza kuondoka leo alfajiri.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally (pichani), alisema kikosi hicho kilichotarajiwa kuondoka saa 10:00 alfajiri, kilitarajiwa kuondoka na wachezaji wake wote akiwamo John Bocco, Victor Akpan na Gadiel Michael ambao tetesi zilisema kuwa wangepelekwa kwenye klabu mbalimbali za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mkopo.



"Tunakwenda na wachezaji wote 19, watakaobaki ni wale tisa tu ambao wapo kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars kinachojiandaa kucheza na Uganda Cranes. Tunakwenda Sudan kwa kupitia Ethiopia ambako tutabadili ndege na kuelekea nchini Sudan," alisema meneja huyo.

Ikiwa Sudan, Simba inatarajia kushuka dimbani Jumapili wiki hii dhidi ya Asante Kotoko ya Ghana ambayo imealikwa pia kwenye michuano hiyo maalum na Agosti 31, mwaka huu itakipiga na wenyeji, Al Hilal.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >